
SportPesa
TZS. 735,865,580
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**HATIMA** shahidi aliyedai kumpa rushwa mil. 90/- Sabaya Jumatatu


Ukurasa 12
KILELE SIKU YA WENYE ULEMAVU
Mwenye ulemavu kijana 'asiyejiweza' asimulia alivyoweza kutoka nyumba ya nyasi, hadi bati

BUFE
IJUMAA DESEMBA 3 2021
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

KILELE SIKU YA WENYE ULEMAVU
Wahusika waorodhesha mapengo walio nayo katika kunufaika na haki za umma
Ukurasa 14

LICHA KUZIDISHIWA LENGO...
NFRA Songea yanunua mahindi 'mpaka basi' shida sasa hifadhi
Na Gideon Mwakanosya, SONGEA

SONGEA imo katika mikoa nane ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula cha Taifa (NFRA) nchini, majukumu ya wakala huyo ni pamoja na kununua na kuhifadhi chakula (mahindi).
Jukumu kubwa la wakala huo katika kununua nafaka, pia chanzo cha mapato kwa halmashauri zote zilizopo mkoani Ruvuma, zikilipa ushuru wa mazao. Pia imekuwa ikitoa ajira ya muda kati ya vijana 300 hadi 600.
Serikali kupitia NFRA imeendelea kununua mahindi ambayo kwa mwaka iliipa Kanda ya Songea kununua jumla ya tani 41,000 za mahindi, kiwango ambacho kimeongezeka ikilinganishwa na msimu uliopita 2020/2021...

...kuona umuhimu wa kutafuta masoko mengine, badala ya kutegemea kuuza mahindi yao NFRA pekee, kwani hawawezi kununua mahindi yote ya wakulima.
Mwaipyana anataja ugumu mwingine unaochelewesha kazi zao, ni ununuzi wa mahindi kutoka kwa wakulima kuwa ni pamoja na uhaba mkubwa wa vifungashio. Hapo anaiomba serikali ichukue hatua za haraka kutatua shida hiyo.
Anasema ili kumaliza ugumu wanahitaji vifungashio 820,000 vinavyoletwa kwa awamu, jambo linalochangia kuwapo kero ya upatikanaji vifungashio vya kuwekewa mahindi, ambayo tayari yameshanunuliwa kutoka kwa wakulima.

RC RUVUMA
Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, anasema mradi wa kununua mahindi unaotekelezwa na NFRA...

UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Desemba 3, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580783
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mvua yaezua nyumba 130

**YANYESHA** kwa dakika 45, baadhi wajeruhiwa, shule, zahanati zakumbwa... *Endelea ukurasa wa 2*



Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Likuyusekamaganga, Wilaya ya Namtumbo, mkoani Ruvuma, akizungumzia jinsi nyumba yake ilivyoezuliwa na mvua iliyoambatana na upepo kijijini hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 4

## DAKTARI: NILIMTIBU MKE WA BILIONEA MSUYA KWA KUDAI KUPIGWA NA POLISI

DAKTARI Deogratius Kalama (36), amedai mahakamani kuwa alimtibu mke wa marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita, baada ya kumweleza ana maumivu ya bega la kushoto na nyonga kwa madai kuwa alipigwa na askari...

UKURASA WA 5

## UBELGIJI KULETA CHANJO 115,200 CORONA LEO

SERIKALI leo inatarajia kupokea chanjo aina ya Johnson & Johnson dozi 115,200 kutoka Ubelgiji ili kuchangia kuongeza kasi ya kampeni ya kuchanja.
Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Ubelgiji...

## Kasi ya 'dadapoa' yamtisha mkuu mkoa

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, alipomtembelea nyumbani kwake, Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kumjulia hali. Rais pia alimtembelea na kumjulia hali Waziri Mkuu mstaafu, Cleopa Msuya nyumbani kwake. **PICHA: IKULU**

# Serikali yatoa hadhari corona wimbi la nne

UKURASA 2

**MICHEZO** KIWANGO SIMBA CHAMKERA PABLO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Kasi ya 'dadapoa' yamtisha RC

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewataka wakuu wa wilaya za Maswa na Bariadi kuweka mikakati ya kudhibiti wanawake wanaojiuza kwa kuwa ni chanzo cha kusambaa kwa Virusi vya Ukimwi.

Aidha, alitaka kuchukuliwa hatua dhidi ya eneo la Malampaka maarufu DAR linalolalamikiwa na kinamama wa eneo hilo kwenye mikutano ya hadhara.

Kafulila alitoa agizo hilo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani iliyofanyika kimkoa wilayani Bariadi, ambaye alihamasisha wanaume kuacha tabia za kupima afya zao kwa kutumia majibu ya mke au mpenzi wake.

Alisema kuwa amepata taarifa kuwa baadhi ya wadada wanajiuza maeneo mbalimbali na kuagiza wakuu wote wa wilaya kuhakikisha maeneo yote yanayotumika kwa biashara ya ngono yanadhibitiwa, kwani hiyo siyo biashara halali na utamaduni wa Watanzania.

Aidha, aliziagiza kamati za amani na za usalama kukutana mara kwa mara na kuhakikisha zinashirikiana katika kudumisha maadili.

"Serikali inaendelea kutumia rasimali watu,fedha na muda kuelimisha jamii kujikinga na Ukimwi, UVIKO16 na magonjwa mengine kwa sababu hakuna maendeleo yatapatikana kama taifa litapoteza nguvu kazi yake kwa vifo vinavyozuilika kwani ushindani wa dunia sasa upo kwenye ubora wa nguvu kazi ambayo inategemewa na kupimwa kwa vigezo hasa viwili, afya na maarifa," alisema.

Kwa mujibu wa Kafulila, asilimia 43 ya maambukizi mapya Tanzania yanatokea kwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 24, hii ndio nguvu kazi ya nchi, na kwamba ni muhimu kuchukua hatua za haraka kwa kua huwezi kujenga taifa la vijana wenye afya dhaifu.

# Mvua yaezua nyumba 130

**Na Amon Mtega,**
NAMTUMBO

NYUMBA 133 za Kijiji cha Likuyusekamaganga, Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma zimeezuliwa na mvua iliyoambatana na upepo na kusababisha familia hizo kukosa makazi. Akizungumzia tukio hilo jana, Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dk. Julius Ningu, alisema mvua hiyo ilinyesha kwa takriban dakika 45 Novemba 30, mwaka huu, kuanzia majira ya saa 10:30 jioni.

Kiongozi huyo alisema tukio hilo limesababisha majeruhi wanane. Kati yao, saba wametibiwa na kuruhusiwa huku mmoja akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo. Dk. Ningu alisema kuwa mbali na makazi ya wananchi, mvua hiyo pia iliezua madarasa matatu na ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Likuyusekamaganga pamoja na zahanati.

Alisema kuwa kutokana na maafa hayo, serikali imepeleka wataalamu ili kufanya tathmini ya uharibifu wote ambao umejitokeza. Baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo, Dk. Ningu alisema serikali itarejesha miundombinu ya shule na zahanati iliyoezuliwa.

Diwani wa Likuyuseka, Kassim Gunda, alisema mvua hiyo imesababisha maafa makubwa, akibainisha kuwa wananchi ambao kwa sasa hawana makazi kutokana na baa hilo, wamejishikiza kwa wananchi ambao nyumba zao hazikuezuliwa wakati serikali ikiendelea na taratibu zingine.

Mwalimu wa shule iliyoezuliwa, Joachimu Komba, alisema uharibifu umetokea zaidi kwenye madarasa na kama hatua za haraka hazitafanyika, hali itakuwa mbaya Januari mwakani wakati ambao wanafunzi wapya wanatakiwa kusajiliwa.



Wananchi kutoka vijiji mbalimbali vya kitongoji cha Nyamongo, wilayani Tarime, mkoani Mara, wakiwa kwenye foleni ya kupima afya zao kupitia mradi wa wiki mbili, uliotekelezwa na Wizara ya Afya kwa ufadhili wa Barrick North Mara uliomalizika katika viwanja vya Shule ya Sekondari ya Nyangoto jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu atoa tahadhari corona wimbi la nne

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka Watanzania kuanza kuchukua tahadhari dhidi ya mlipuko wa virusi vya corona wimbi la nne ambalo limeanza kuzitesa baadhi ya nchi hivi sasa.

Majaliwa alitoa hadhari hiyo jana jijini Dodoma alipokuwa akizindua ujenzi wa ofisi za wizara katika mji wa kiserikali Mtumba pamoja na maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru wa Tanzania Bara kitaifa.

Alisema hivi sasa kumeibuka kwa wimbi la nne la mlipuko wa virusi vya corona katika baadhi ya mataifa, hali ambayo inahitaji wananchi kuanza kuchukua tahadhari dhidi ya janga hilo la UVIKO-19.

"Baadhi ya nchi zimeanza kupata wimbi la nne la mlipuko wa virusi vya corona tusiruhusu kuingia kwa wimbi hili nchini mwetu... tunachopaswa kufanya ni kuhakikisha kuwa tunazingatia maelekezo ya wataalamu wetu wa afya.

"Lakini tuliingiza chanjo nchini, nitume nafasi hii kuwasihi Watanzania kuhakikisha mnakwenda kupata chanjo kwani inasaidia sana kuongeza virutubisho ambavyo vinaweza kukabiliana na ugonjwa huu... mimi tayari nilishachanja na niko fiti, watu wengi pale mwanzo walikuwa na hofu lakini kama mnavyoona tuliochanja tuko fiti hivyo ambao bado tukitoka hapa twende tukachanje," alisisitiza Majaliwa.

**WALIOPATA MIMBA KURUDI SHULE**

Akizungumzia kuhusu waraka uliotolewa na serikali juu ya wanafunzi waliokatisha masomo kutokana na ujauzito kuruhusiwa kurudi shule, aliwataka viongozi kusimamia jambo hilo ili lifanikiwe.

"Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni alitoa kauli ya kuweka usawa hasa kwa watoto wa kike kupata elimu wale ambao walikosa fursa kutokana na sababu mbalimbali, hivyo basi ni wajibu wetu kujipanga kuhahakikisha jambo hili linafanikiwa,"alisema Majaliwa.

Aidha, alisema serikali itatoa maelekezo maalum juu ya utekelezaji wa jukumu hilo ili liweze kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

**SENSA 2022**

Pia aliwataka Watanzania kujiandaa na zoezi la sensa ya watu na makazi linalotarajiwa kufanyika Agosti mwakani.

"Tarehe rasmi tutatangaza, lakini leo nawakumbusha kuwa ikifika wakati tutoe ushirikano ili kuiwezesha nchi yetu kupata takwimu sahihi zitakazotumika kwa ajili ya kufanya mipango ya maendeleo katika eneo husika,"alisema Majaliwa.

**UJENZI WA OFISI**

Kuhusu uzinduzi wa ujenzi wa ofisi za wizara awamu ya pili, alisema anamshukuru Rais Samia kwa kuidhinisha kiasi cha Sh. bilioni 300, kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

"Tunatarajia hadi kukamilika kwa ujenzi huu hakutakuwa na mtumishi hata mmoja atakayebaki jijini Dar es Saalam, hivyo niagize kuwa ujenzi huu ujengwe kwa kuzingatia maelekezo na kwa ubora,"alisema.

Alisema majengo yanayotumika sasa yalikuwa ni ya muda ambayo ujenzi wake ulichukua muda wa miezi minne hadi kukamilika.

"Ujenzi huu wa awamu ya pili utakuwa na majengo ya ghorofa kuanzia tatu na kuendelea majengo yapatayo 24," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Ajira, Kazi, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema kuwa hadi sasa jumla ya watumishi 18,300 wameshahamia Dodoma na zaidi ya Sh. bilioni 168 zimeshatumika.

Mhagama, alisema majengo ambayo watumishi waliacha Dar es Saalam, serikali ilizipatia taasisi za umma ambazo zilikuwa hazina ofisi, hali iliyosaidia kupunguza gharama katika nyumba za kukodi.

"Taasisi zipazo 54 zilipatiwa majengo yapatayo 18 na kuzisaidia kuondokana na kukodi majengo binafsi hali iliyosaidia kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 10.4 zilizokuwa zinalipwa," alisema Mhagama.

HABARI KITAIFA

# Hatima shahidi aliyedai kumpa milioni 90/- Sabaya Jumatatu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha inatarajiwa Jumatatu kutoa uamuzi kama mfanyabiashara Francis Mroso (44) akamatwe kutokana na ombi la wakili wa utetezi kwa kuwa shahidi alidai alitoa rushwa ya Sh. milioni 90.

Katika kesi hiyo, Mroso ni shahidi wa 10 wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya.

Jana mahakama hiyo ilitoa muda kwa mawakili wa upande wa mashtaka kujibu hoja zilizowasilishwa na upande wa utetezi mahakamani huko.

Juzi Wakili wa Utetezi, Fridolin Bwemelo, aliwasilisha ombi la kukamatwa kwa shahidi huyo, Mroso, akidai kwamba alitoa rushwa ya Sh. milioni 90 na yupo uraiani na aliowapatia rushwa ni washtakiwa kwenye kesi hiyo.

Alidai mahakamani huko kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 15(1B), inaweka wazi hatua za kuchukuliwa dhidi ya mtu atakayetoa na kupokea rushwa na hakuna kifungu kinachoeleza kuna rushwa ya kulazimishwa kutoa.

Wakili huyo alidai kuwa kwa mujibu wa kifungu hicho, hakuna sehemu kimezungumzia suala la kutoa rushwa kwa kulazimishwa kwa kuwa mtoaji na mpokeaji wa rushwa ni wakosaji.

Vilevile, wakili huyo aliomba kupata tafsiri ya mahakama kwa kuwa kesi ilifunguliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na ilitakiwa kuendeshwa na mawakili wake badala ya mawakili wa serikali kama ilivyofanyika.

"Mheshimiwa hakimu tunajiuliza ni kwa nini mtu aliyetoa rushwa na kukiri mbele ya mahakama hii bado yupo huru, lakini waliopokea rushwa wameshtakiwa na wapo ndani, maombi yetu ili kuondoa utata kwenye jamii inayotuzunguka tunaomba shahidi huyu akamatwe. "Jamii yetu yenye sera ya kazi iendee na kuepuka upendeleo kwa kuwa kupitia hayo ili jamii ielewe kwamba haki inatendeka kwa watu wote, hivyo tunaiomba mahakama kupitia sheria ya makosa ya jinai inaweza kutoa amri ya kumkamata mtu yeyote aliyekiri makosa mbele yake kwa kutenda kosa hilo," alidai.

Wakili huyo alidai kwamba mahakama imejiridhisha kupitia kwa shahidi ambaye yupo chini ya kiapo na kukiri kwamba alitoa rushwa ya Sh. milioni 90.

Awali mawakili wa Serikali Filex Kwetukia, Tersila Gervas, walidai watawasiliana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali (DPP) ili kutoa ufafanuzi kwa nini walipewa ridhaa ya kusimamia kesi hiyo badala ya TAKUKURU.

"Tunaomba wiki mbili tuwasiliane na DPP aliyetutuma kufanya kazi hii kwa sababu hata sisi tumetuhumiwa pia kwamba hatuna sifa ya kusimamia kesi hii," alidai Tersila.

Hata hivyo, akijibu hoja za mawakili wa utetezi, Wakili wa Serikali Mwandamizi huyo, Tersila, alidai kwamba kwa mujibu wa katiba ya nchi, ibara ya 59B imempa mamlaka DPP, kuendesha mashauri yote ya jinai.

Alidai kwamba sheria imeeleza DPP anaweza kutoa mamlaka kwa wasaidizi wake, wakiwamo mawakili waandamizi wa serikali kuendesha mashauri hayo kwa niaba yake. "Katika nchi yetu mamlaka ya uchunguzi yapo chini ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), lakini baada ya serikali kuona kuna umuhimu polisi kuchunguza na baadaye walihamishia kwenye taasisi zingine, ikiwamo TAKUKURU kufanya uchunguzi kwa kuwa taasisi hii inatambulika kisheria na ilifanya uchunguzi wa shauri hili na kupeleka kesi mahakamani baada ya upelelezi kukamilika," alidai Tersila.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai mahakamani kwamba ombi la kukamatwa kwa Mroso limepelekwa kinyume cha kifungu cha 17 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa kuwa ilitakiwa kusomwa pamoja na kifungu cha 13 cha sheria hiyo. Alidai kwamba mbele ya mahakama hiyo, hakuna hati ya mashtaka ya Mroso, bali amesimama kama shahidi wa mashtaka dhidi ya Sabaya na wenzake sita.

"Kifungu cha 9A cha Sheria ya Huduma ya Mashtaka kinampa mamlaka DPP kuamua nani ashtakiwe na yupi asishtakiwe. Kwa msingi huo, maombi yaliyoletwa mahakamani yatupiliwe mbali kwa kuwa hayana miguu, hayajazingatia matakwa ya kisheria," alidai.

Baada ya majibu hayo, Hakimu Kisinda aliahirisha kesi hiyo hadi Jumatatu atakapotoa uamuzi mdogo.

# Mawaziri 2 kupiga kambi kusaka wanaofanya ukatili

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia ya Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeahidi kupiga kambi ya pamoja katika mikoa iliyoshamiri kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake kuhakikisha vinakoma katika maeneo hayo.

Mpango huo ulitangazwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia ya Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, wakati akifungua kituo cha pamoja cha Mkono kwa Mkono katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan mkoani Morogoro.

Alisema kwa kuanzia, atanza na mkoa wa Morogoro ili kuungana na Mkuu wa Mkoa huo, Martine Shigela, ambaye tayari ametangaza vita hiyo kutokana na takwimu za vitendo vya ukatili kwa watoto kuwa juu.

"Nataka kukuhakikisha Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, tutaanza na mkoa wako kuweka kambi hapa, mimi pamoja na Waziri wa TAMISEMI, tutapita kata zote za wilaya zenye matitizo ya ukatili wa aina zote na wahusika wote tutachukua hatua kali ili kukomesha kabisa tatizo hili la ukatili," alisema Dk. Gwajima. Waziri huyo wa Afya, alisema Madawati ya Jeshi la Polisi ya Jinsia nchini yamepokea na kushughulikia jumla ya mashauri 20,025 ya ukatili ukilinganisha na mashauri 18,270 yaliyoripotiwa mwaka 2019/20.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa huduma katika vituo 14 vya mkono kwa mkono nchini katika hospitali za serikali za Amana, Mwananyamala, Tumbi, Iringa, Sekou Toure, Mbeya FFU, Simiyu, Shinyanga, Kahama, Hai, Kitete, Mount Meru, na Nindo.

Alisema katika kipindi cha Julai 2020 - Juni 2021 ,waathirika 1,857 wa ukatili wa kijinsia walipata huduma kati yao watoto 1,072 wavulana wakiwa 412 na wasichana wakiwa 660 huku wanawake wakiwa 785.


NMB Karibu yako

TAARIFA KWA UMMA

Mpendwa Mteja,

Tunaomba kukutaarifu kuwa benki imefanya mabadiliko kadhaa katika gharama na ada za huduma zifuatazo kuanzia **tarehe 3 Januari 2022**.

| Aina ya Ada | Wigo | Gharama (TZS) |
|---|---|---|
| Kuhamisha Fedha NMB kwenda NMB kwa NMB Mkononi | 0-9999 | 50 |
| | 10,000-29,999 | 100 |
| | 30,000-99,999 | 450 |
| | 100,000-499,999 | 1,000 |
| | 500,000-5,000,000 | 1,300 |
| Kutoa Fedha kwa NMB Wakala | 1,000 - 4,999 | 300 |
| | 5,000 - 9,999 | 750 |
| | 10,000 - 19,999 | 1,200 |
| | 20,000 - 39,999 | 1,650 |
| | 40,000 - 49,999 | 2,000 |
| | 50,000 - 99,999 | 3,500 |
| | 100,000 - 199,999 | 4,500 |
| | 200,000 - 299,999 | 5,500 |
| | 300,000 - 599,999 | 6,500 |
| | 600,000 - 799,999 | 7,000 |
| | 800,000 - 999,999 | 7,500 |
| | 1,000,000 - 2,999,999 | 8,000 |
| | 3,000,000 - 4,999,999 | 9,500 |
| | 5,000,000 - 5,999,999 | 9,800 |
| | 6,000,000 - 6,999,999 | 10,700 |
| | 7,000,000 - 7,999,999 | 12,600 |
| | 8,000,000 - 8,999,999 | 13,900 |
| | 9,000,000 - 10,000,000 | 15,000 |
| Kutoa fedha katika ATM za NMB | 1,000-19,999 | 1,100 |
| | 20,000-39,999 | 1,200 |
| | 40,000-99,999 | 1,300 |
| | 100,000-199,999 | 1,400 |
| | 200,000-400,000 | 1,500 |
| Kurejeshewa PIN ya Kadi ya ATM | TZS 3,000 | |

Kwa taarifa zaidi, tafadhali piga **0800 002 002** au tutumie barua pepe kupitia: **tuambie@nmbbank.co.tz**

**Imetolewa na Utawala wa NMB Bank Plc.**

www.nmbbank.co.tz

216598402

# Daktari: Nilimtibu mke wa Bilionea Msuya kwa kudai kupigwa na polisi

**Na Hellen Mwango**

DAKTARI Deogratius Kalama (36), amedai mahakamani kuwa alimtibu mke wa marehemu Erasto Msuya, Miriam Mrita, baada ya kumweleza ana maumivu ya bega la kushoto na nyonga kwa madai kuwa alipigwa na askari polisi.

Dk. Kalama alitoa ushahidi wake jana katika kesi ndogo ndani ya kesi ya msingi ya mauaji ya Anethi Msuya inayomkabili Mrita na mwenzake Revocatus Muyella.

Ushahidi huo unasikilizwa katika Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam iliyoketi chini ya Jaji Edwin Kakolaki.

Shahidi alidai kuwa Januari 18,2017 alipokuwa ofisini kwake hospitali ya wilaya ya Temeke, walifika askari na wagonjwa wawili mwanamke na mwanamme.

"Nilimsikiliza mgonjwa mwanamke ambaye ni yule pale (alimwonyesha kwa kidole mshtakiwa Mrita), alinieleza anasumbuliwa na maumivu bega la kushoto na nyonga kwa kuwa alipigwa na polisi miezi kadhaa iliyopita," alidai na kuongeza:

"Nilimwandikia vipimo ikiwamo Ex-ray ili nijiridhishe kama ana majeraha kwa ndani, lakini majibu yalionyesha ni maumivu tu ya kawaida, ambayo yanaweza kumpata hata mtu aliyefanya mazoezi" alidai Dk. Kalama.

Akihojiwa na Wakili wa utetezi, Omary Msemo, kama alimsikiliza mgonjwa huyo huku askari wakiwa chumba cha daktari, shahidi alidai wakati anatoa huduma askari walikuwa nje ya mlango wa chumba chake.

Jaji Kakolaki alisema kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa siku tatu na kwamba itaendelea tena Machi, 2022 Msajili atakapopanga tarehe ya kuendelea kusikiliza utetezi wa kesi hiyo ndogo ndani ya kesi ya msingi.

Alisema washtakiwa warudishwe mahabusu mpaka mwakani.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa wote wanakabiliwa na shtaka la kumuua kwa makusudi Aneth Msuya, dada wa marehemu bilionea Erasto Msuya Mei 25, 2016 eneo la Kibada Kigamboni, jijini Dar es Salaam.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella (katikati), akifurahia jambo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya I&M, Baseer Mohammed (kulia) na Meneja wa Wateja wa Rejareja wa benki hiyo, Lilian Mtali (wapili kushoto), wakati wa uzinduzi wa tawi jipya la Benki ya I&M, jijini Arusha mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yapongezwa utalii duniani

**Na Mwandishi Wetu,**
MADRID, HISPANIA

TANZANIA yapongezwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani (UNWTO), kwa namna limefanikisha onyesho la kwanza la utalii katika nchi za Afrika Mashariki, lililofanyika Oktoba, mwaka huu, jijini Arusha kwa lengo la kutangaza utalii katika nchi za jumuiya.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Katibu Mkuu wa shirika hilo, Zurab Pololkashvir, wakati akitaja baadhi ya nchi za Afrika ambazo licha ya changamoto ya ugonjwa wa UVIKO-19, lakini zimeendelea kufanya vizuri katika suala la utalii.

Kiongozi huyo alitaja baadhi ya mafanikio yake kwa kipindi cha uongozi wake tangu alipochaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa UNWTO katika siku ya pili ya Mkutano Mkuu wa 24 wa UNWTO ulipoanza.

Alisema Tanzania ni kati ya nchi za Afrika zinazochipukia katika kuhakikisha sekta ya utalii inafanya vizuri kwa kuchangamkia fursa mbalimbali ambazo zimekuwa zikijitokeza kwa ajili ya kutangaza vivutio vyake vya utalii. Alitaja onyesho la kwanza la Utalii la Afrika Mashariki (EARTE) kuwa Tanzania imeonyesha ukomavu na ujasiri wa hali ya juu katika kulifanya kwa mafanikio makubwa onyesho lile licha ya kuwa na muda mfupi wa maandalizi na uwepo wa changamoto ya ugonjwa wa UVIKO -19.

"Kati ya nchi za Afrika ninazoziona zinakwenda kuongoza kimapato kwa kuifanya sekta ya utalii kuwa namba moja huwezi kuiacha kuitaja Tanzania "am so proud of you" (najivunia juu yako) Tanzania," alisema Katibu Mkuu wa UNWTO," Zurab.

Akizungumzia pongezi hizo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amemshukuru Katibu Mkuu wa UNWTO, Zurab kwa kuona na kukubali jitihada mbalimbali zinazofanywa na Tanzania katika kuhakikisha sekta ya utalii inaendelea kufanya vizuri kimapato.

"Tumepongezwa kwa namna ambavyo tumeweza kufanya onyesho la kwanza la utalii katika nchi za Afrika Mashariki. Sisi tuliona dogo, lakini wenzetu huku katika nyanja za kimataifa waliliona kubwa," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema onyesho la EARTE pamoja na mkutano huu wa UNWTO kwa nchi ya Tanzania ni fursa ya kuweza kutangaza utalii, lakini kama fursa ya kuwavuta wenzetu watalii waje pia nchini Tanzania katika kuwekeza kwenye sekta ya utalii.

Dk. Ndumbaro amesema pongezi hizo zinatia moyo ya kuongeza kasi zaidi katika kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania.

"Tumepongezwa na nimesema kwamba kumbe kweli watanzania wanaweza kufanya mikutano kwa kiwango kikubwa zaidi," alisema Dk. Ndumbaro.

Kupitia pongezi hizo, Dk.Ndumbaro alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa ushirikiano mkubwa anaoupata kutoka kwake huku akitaja kampeni maalum ya kutangaza utalii kwa kupitia kipindi cha 'Royal Tour' aliyoiasisi yeye mwenyewe kuwa hali hiyo inampa nguvu zaidi katika kutangza utalii wa Tanzania ndani na nje ya nchi.

# NCCR yaipa serikali mbinu kukabili corona

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimeishauri serikali kuwa na meza ya mazungumzo na wadau kupata mbinu mpya za kukabiliana na matatizo mbalimbali yanayolikabili taifa ikiwamo ugonjwa wa UVIKO-19.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Taifa wa NCCR-Mageuzi, James Mbatia, alisema taifa limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo hadi sasa hazijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Alishauri kuwa nchi ionyeshe ushirikiano na siyo ushindani katika suala la kinga, utayari na mwitikio katika kupambana na janga hilo ili kuweza kulikabili kwa maslahi ya kulinda afya za Watanzania.

"Duniani leo tatizo hili la virusi vinavyosababisha ugonjwa wa UVIKO-19 kuna hiki kilichogundulika kama wiki mbili zilizopita, jana, juzi Shirika la Afya Duniani (WHO), lilisema kama dunia ilishindwa kupambana na kirusi aina ya Delta, je, hiki kipya tutakiweza hiyo ni lugha ya dunia.

Aliwashauri viongozi kuwa wawe mstari wa mbele na mfano wa kuigwa katika kupambana na tatizo hilo.

Kwa mujibu wa Mbatia, dunia iko mbioni kuja na mkataba wa kidunia katika kulinda afya za watu dhidi ya janga hilo huku akiwaasa viongozi kuwa waache kuongea wanavyojua bali wakubali kufuata ushauri wa wataalamu.

Alisema NCCR-Mageuzi inaomba ushirikiano wa Watanzania na dunia katika kupambana na jambo hilo kwa kuwa na utayari, na alitoa wito kwa wasiopata kinga waweze kuchanja ili kulinda afya zao.

"Kuna viongozi wengine wanasimama kwenye majukwaa wanazungumzia UVIKO-19, lakini wenyewe hawajachanja. Mimi binafsi ninajiamini kuzungumzia hili kwa kuwa nilichanja hadharani na familia yangu na viongozi wote wakuu wa chama, kuonyesha kuwa kiongozi ni kuwa kielelezo," alisema Mbatia.

Pia alishauri kuwa nchini kila baada ya wiki kutolewe takwimu zinazoonyesha ni watu wangapi wamechanjwa.

# Sekta binafsi Tanzania, Uganda wakubaliana mambo 10 uwekezaji

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) na Taasisi ya Sekta Binafsi Uganda (PSFU) zimekubaliana mambo 10 makubwa kuhusiana na fursa zilizopo katika gesi na mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta linalojengwa kati ya Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPSF, Angelina Ngalula akisoma makubaliano hayo jana jijini Dar es Salaam, alisema wameona ushirikiano kati ya sekta hizo binafsi ni muhimu ili pande zote mbili zinufaike na mradi huo.

Alisema makubaliano hayo yanatokana na kongamano la siku mbili lililokutanisha taasisi hizo kuanzia Novemba 27 jijini Dar es Salaam kujadili fursa kwenye bomba la mafuta na gesi.

"Msisitizo uliwekwa kwa kampuni kubwa ambazo zitapata bahati kupata zabuni kufanya kazi kwa kushirikiana na biashara ndogo na za kati (SME) ili kuibua fursa na kusaidia kujenga mnyororo wa thamani," alisema.

Eneo la pili alilitaja ni ushirikiano wa kufanya kazi kwa karibu na wanachama wao ili kuhakikisha mafunzo sahihi yanatolewa yatakayowezesha kuwapo kwa bidhaa bora zitakazozalishwa.

"Eneo la tatu tumejadili umuhimu kwa sekta binafsi kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi muhimu za serikali katika maeneo muhimu kama vile vifaa vya kuinulia mizigo bandarini," alisema.

Ngalula alisema eneo la nne ni kueneza fursa na uelewa kuhusiana na mradi huo kwa wananchi na la tano ni uelewa wa masuala ya fursa za ubia kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati.

"Eneo la sita ni uwezo wa kukidhi viwango na matakwa yanayotakiwa kwenye mradi kwa kuwasaidia wajasiriamali kukidhi matakwa ya ubora ili kunufaika nao. Hali ilivyo sasa ni wafanyabiashara wengi wadogo na wa kati kukosa uwezo wa kukidhi mahitaji ya vigezo vya ubora," alisema.

Ngalula alisema eneo la saba ni ukosefu wa ujuzi stahiki na kushauri vyuo na mifumo ya elimu kufanya kazi kwa karibu na sekta binafsi ili kutambua mahitaji ya kiujuzi yanayotakiwa kwenye miradi mikubwa.

Alisema eneo la nane ni upatikanaji wa mitaji kwa wafanyabiashara ambao utawawezesha kushiriki kikamilifu katika kuzichangamkia fursa.

"Eneo la tisa tumesisitiza kuwa kuwapo na mazungumzo mengo baina ya serikali hizi mbili, sekta hizi binafsi na baina ya sekta binafsi na serikali Sasa maneno yaliyojadiliwa hayo yawe kwa vitendo. Kumi, ushiriki wa wazawa nalo tumelijadili kwa kina tumeziomba serikali hizi kuangalia upya sheria hii.

"Upande wa Uganda kampuni inatambulika ni kampuni asili hata kama inaongeza thamani ya bidhaa, Tanzania kampuni ya asili ni kampuni ambayo ina hisa zaidi ya asilimia 51 kwa Mtanzania," alisema.

Ngalula alisema matatizo matano ambayo wanaiomba serikali isaidie ni pamoja na ushirikiano wa sekta binafsi kwenye mazungumzo ya awali kabla na baada ya kutiwa saini mikataba na wawekezaji.

# Ubelgiji kuleta chanjo 115,200 corona leo

**Na Romana Mallya**

SERIKALI leo inatarajia kupokea chanjo aina ya Johnson & Johnson dozi 115,200 kutoka Ubelgiji ili kuchangia kuongeza kasi ya kampeni ya kuchanja.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Ubalozi wa Ubelgiji na kuthibitishwa na serikali ya Tanzania, chanjo hizo zitachangia kuongeza kasi ya kampeni ya chanjo nchi nzima ili kulinda maisha na afya za Watanzania.

"Usambazaji wa chanjo hufanyika kupitia msambazaji wa kimataifa COVAX, na kuratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto ( UNICEF).

"Mchango huu ni sehemu ya ahadi ya awali ya Serikali ya Ubelgiji ya kusambaza angalau chanjo milioni nne kwa nchi za kipato cha kati na chini kufikia mwisho wa mwaka huu."

Taarifa hiyo ilisema Ubelgiji imetekeleza ahadi hiyo na hadi kufikia sasa imetoa chanjo milioni tisa kupitia COVAX, pamoja na mchango wake wa kifedha wa EURO milioni 12.

Ilisema chanjo ya UVIKO-19 hupunguza hatari ya maambukizi pamoja na matatizo yake yanayoweza kuwa makubwa.

"Iwapo watu wengi iwezekanavyo Tanzania watapewa chanjo, kuenea kwa virusi hivyo kutazuilika. Tunaipongeza serikali kwa kuzidisha kampeni za kuongeza uelewa ili kuwafahamisha wananchi kwa ujumla kuhusu umuhimu wa kupata chanjo na kuwezesha kupatikana nchi nzima," ilisema.

Taarifa hiyo ilisema upatikanaji wa chanjo ya UVIKO-19 Tanzania bado ni mdogo na ni chini ya wastani wa Afrika. "Kwa ombi la Waziri wa Ushirikiano wa Maendeleo, Meryame Kitir, mlengo wa nchi yetu wa kutoa michango baina ya nchi mbili utakuwa Afrika na hasa zaidi kwa nchi washirika wa Afrika, ambapo upatikanaji wa chanjo unakosekana sana," ilifafanua.

Ilisema wakati Ubelgiji na nchi nyingi za Magharibi sasa zina viwango vya kuridhisha vya chanjo, kwa wastani barani Afrika karibu asilimia tano ya watu wamechanjwa.

Kaimu Mkuu wa Mawasiliano Idara ya Afya wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Catherine Sungura, alithibitishia Nipashe kuwa serikali leo inatarajia kupokea msaada huo wa chanjo kutoka Ubelgiji.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI HUDUMA NA KUFUNGA (PAMOJA NA UTOAJI WA MAFUNZO KWA MTUMIAJI) MTANDAO WA KUTOA TAARIFA.**
**KUMBUKUMBU: 0010007310**

Kampuni ya Kimataifa ya Mafuta na Gesi ya TotalEnergies East Africa Midstream B.V, inahitaji huduma za kampuni au shirika lililo na uzoefu uliothibitishwa wa kuunda,kusakinisha,na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mwisho kwa huduma inayofuata ya dawati la usaidizi na kwa mfumo wa kuripoti maudhui ya ndani ya mtandao (LCRP) kwa ajili ya mradi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:**

Mradi wa EACOP unahitaji watoa huduma wenye uzoefu na uwezo yakinifu wa kutoa huduma za kutengeneza na kusimika mfumo wa Mtandao wa kutoa taarifa (LCRP) unaokidhi hitaji na vigezo vifuatavyo:

- Mfumo unaohifadhi taarifa katika mtandao na unaoweza kuzuia ufikikaji katika baadhi ya vipengele kwa watoa huduma na mashirika kwa kuwa na nenosiri litakalo tolewa na Mradi wa EACOP Pamoja na nenosiri linaloweza kudhibitiwa..
- Inayoruhusu usajili wa watoa huduma wa nchini Uganda na Tanzania kuweza kupata taarifa kuhusu taarifa ya ombi la Kuonesha Nia (EOI).
- Inayowezesha wasambazaji kutoa ripoti ya mafanikio na maendeleo ya Watoa huduma wa ndani katika fomu zinazolindwa na nenosiri na zinazo iwezesha EACOP kutizama mwendendo wa wasambazaji kwa kulinganisha na taarifa za siku ya kikomo.
- Uwezo wa kuchanganua data ya maudhui ya muuzaji ,msambazaji, wa ndani na kuandaa ripoti kwa kuzingatia matakwa ya mamlaka yan chi za Tanzania na Uganda na kuchambua mwenendo kwa kulinganisha na matarajio.
- Watoa huduma wanahimizwa kuelezea uwezo wowote wa ziada wa utendaji uliopo au unaowezekana kuwa na manufaa kwa EACOP, na uwezo wake wa kujenga uwezo kwa watoa huduma .
- Uwasilishaji wa ana kwa ana au kwa kutumia Programu kwa watumiaji na watoa huduma kwa kutumia lugha zaidi ya moja.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni au mashirika yanayoonyesha nia yao yanahitajika kuwasilisha taarifa zifuatazo:

- Rekodi ya kina ya utendakazi, na uwezo wa kutengeneza na kusimika programu ya computer inayoweza kukidhi hitaji na inayotuza taarifa katika mtandai, kufundisha watumiaji na kuwa na lugha zaidi ya moja (hususani Kiswahili na Kiingereza), dawati la usaidizi kwa Tanzania na Uganda, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa.
- Wafanyakazi wanaokidhi na wenye uzoefu wa kuweza kuelewa mahitaji ya Mradi wa EACOP kwa kuzingatia sheria za Watoa Huduma wa nchini Tanzania na Uganda na kutengeneza programu ya kompyuta.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia au
  Uthibitisho wa usajili katika Kanzi Data ya watoa Huduma wa ndani nchini Uganda wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za nchini Tanzania/Uganda pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, usalama na Mazingira, taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani vya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa leseni ya usajili kutoka kwa mamaka husika nchini Tanzania/Uganda kwa ajili ya utoaji wa huduma tajwa.
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha pamoja na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **eacop-tz.eoi.1000001@totalenergies.com** (ukubwa wa barua pepe 20 Mb) saa au kabla ya saa **11** Jioni Afrika Mashariki (EAT) tarehe **23rd, December 2021.** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007310**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia iii kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo iu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tuzuie maambukizi ya VVU kwa vijana

**JUZI** ilikuwa ni maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya, ambayo katika taarifa za utafiti zilionyesha kuwa maambukizi mapya kwa vijana kati ya miaka 15 hadi 24 yamezidi kuongezeka huku wasichana wakiwa vinara katika janga hilo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Ajira, Uratibu wa Bunge, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema tafiti hizo zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ya VVU yanawakabili zaidi vijana wenye umri huo ambayo yamefikia asilimia 40.

Aidha, asilimia 80 kati ya hao ni vijana wa kike ambao ni nguvu kazi ya taifa na kwamba katika kukabiliana na hali hiyo serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ukiwamo wa kudhibiti Ukimwi wa mwaka 2018/19 na 2022/23.

Lengo la mpango huo ni kupunguza maambukizi mapya ya VVU, kupunguza vifo vitokanavyo na VVU na kuhakikisha watu wanaoishi na maambukizi ya VVU wanaendelea kutumia dawa.

Pia, alitaka mikoa inayoongoza kwa maambukizi ni Njombe, Iringa, Mbeya, Kagera na Geita huku baadhi ikiwa na kasi kubwa ya maambukizi zaidi ambayo ni Geita, Simiyu, Manyara na Dodoma.

Miongoni mwa jitihada zinazofanywa ni kusambaza kondomu kwenye maeneo ya migodi na uvuvi ikiwamo kutoa elimu ya kujikinga.

Ongezeko hilo la maambukizi kwa vijana siyo habari njema kabisa, bali ni jambo la kushtua linalopaswa kuangaliwa kwa jicho la ziada ili kuhakikisha maambukizi yanashuka au yanakwisha kabisa na kufikia lengo la 2030.

Unapotembelea maeneo mengi ya starehe kama ni bar au disco likiwa ni jipya kidogo kidogo litaanza kupata wadada wanaojiuza ambao ukiwaangalia kwa haraka wako kwenye umri mdogo sana, kiasi cha kujiuliza wazazi au walezi wanajua kinachoendelea dhidi ya watoto wao?

Wasichana hao huwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume tofauti tofauti wengine ni wenye umri sawa na wazazi wao, na wanapotoka hapo huwa na uhusiano na vijana wa umri wao au waliwapita kidogo.

Mathalani, Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ameeleza kukerwa na kuongezeka kwa dada poa, huku akiagiza Wakuu wa Wilaya kuchukua hatua kukomesha hali hiyo.

Uwepo wa dada poa hawa kumefanya ionekane ni jambo la kawaida sana kufanya ngono holela na hadharani, kiasi kwamba unapotembelea mji au jiji lolote unaelekezwa wanapopatikana kiurahisi. Mbaya zaidi panapofanyika uchafu huo ni mahali ambako kuna uongozi kuanzia ngazi ya mtaa hadi wilaya, ambao wangesimama imara ingesaidi kuwaondoa, lakini wamiliki wa sehemu za starehe wanaona hao wanawasaidia kuvuta wateja ambao ni wanaume.


Ni muhimu takwimu hizi zikatumiwa na wadau mbalimbali kutoa elimu sahihi kwa vijana kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu, lakini kila halmashauri kutoa mtaji na elimu ya ujasiriamali kwa vijana ili wanapomaliza masomo wasikae mtaani bali wajishughulishe na kazi za uzalishaji.

Tunaamini kwa sasa watu wanauchukulia poa Ukimwi tofauti na miaka ya nyuma, sasa ni wakati wa kuongeza kasi ya kutoa elimu sahihi kwa vijana waepuke kuingia kwenye ngono zembe kabla ya umri na wakati sahihi kwenye maisha yao.

Pia ni muhimu elimu ya msingi hadi Chuo Kikuu ikamwandaa kijana kujitegemea kwa kuwa wengi wanaojiuza hutafuta kipato cha kujikimu, na tunaamini kama watajikomboa dhidi ya umaskini na fikra watajitegemea kimaisha.

Bila kuwekeza nguvu kukomboa kundi la vijana kuna hatari kubwa ya maambukizi kuzidi zaidi hasa kwa wanandoa kwa kuwa baadhi huwa na mahusiano na waume au wake za watu ambao huenda kukutana na wenzao wao na kusambaza maambukizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Shida ya maji iwe chachu mpya ya kupanda miti

Na Jenifer Gilla

**MGAWO** wa maji uliokumba baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam na mikoa mingine kwa takribani wiki tatu sasa, unaendelea kuwakosesha raha wakazi wake, hususani ambao ndio wahusika wakuu wa kusaka maji.

Hali ni mbaya zaidi ikwa kinamama wanaoishi nyumba ambazo hazina mabomba ya maji, wanatumia muda mrefu hivyo hutumii saa nyingi zaidi kusaka maji, ili kukidhi mahitaji ya familia zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Mazingira (DAWASA), Cyprian Luhemeje, alipokuwa anatoa taarifa ya mgawo huo, alisema shida itayakumba maeneo yote ya jiji, kila eneo linaweza kukosa huduma hiyo siyo chini ya saa 12, chanzo kikiwa ni kushuka kwa kina cha maji cha Mto Ruvu.

Ingawa mvua zinazoendelea kunyesha zinaonyesha matumaini ya kupunguza kadhia hiyo, lakini ukweli wa mambo ni kuwa bado haijafahamika mgawo huo utafikia tamati wakati gani, kwa kuwa mwenendo wa mvua si wa kuridhisha.

Kama hali ikiendelea kuwa hivi, inaweza kuathiri hadi sekta ya nishati ya umeme, kwa kuwa chanzo chetu kikuu cha kuzalisha umeme unaoweza kugharamiwa na mwananchi wa hali ya chini ni maji.

Tanzania kwa sasa imeanza kupata athari mabadiliko ya tabianchi kwa kiwango cha juu, ukilinganisha na miaka ya nyuma, tunaona kuwa hakukuwa na mvua ya kutosha iliyozoeleka hali iliyosababisha kina cha Mto Ruvu kupungua.

Si hivyo tu, hali ya hewa nayo si rafiki, kumekuwa na jua kali linalosababisha joto kuwa hali inayosababisha uhitaji wa maji kwa wanadamu kuongezeka, sasa wakati binadamu anahitaji maji zaidi nayo hayapatikani.

Si hivyo, tu mabadiliko hayo yanaleta athari katika sekta nyingine muhimu ikiwamo ya chakula, hivi karibuni, Waziri wa Kilimo nchini Tanzania, Profesa Adolf Mkenda, wakati akizungumza katika tathmini ya wizara yake tangu nchi hiyo ijipatie uhuru, alisema kuwa utoshelevu wa chakula katika msimu huu utashuka hadi asilimia 107 kutoka asilimia 125 zilizofikiwa.

Alifafanua kuwa upungufu wa chakula umetokana na ukosefu wa maji na hii imetokana na mvua iliyotegemewa inyeshe mwezi wa tisa haikunyesha na Mamlaka ya Hali ya Hewa ilitolea ufafanuzi suala hili.

Athari za mabadiliko ya tabianchi zinatokana na ukataji wa miti uliofanywa kwa kiwango kikubwa nchini hali inayosababisha kutokuzalishwa kwa oksijeni ya kutosha kusafisha na hewa chafu (gesi ukaa) inayozalishwa inayoendelea kuharibu tabaka la juu angani 'ozone layer' na kusababisha miale ya jua kupiga moja kwa moja kwenye anga na ardhi duniani.

Kazi ya miti ni kutoa hewa safi ambayo husafisha hewa chafu inayozalishwa na viwanda vikubwa, pamoja na mambo mengine ambayo yasipodhibitiwa yataendelea kuharibu tabaka hili muhimu kwetu.

Hapo inaruhusu miale ya jua mingi zaidi, kufika duniani na athari yake ni hali ya joto kuongezeka kuliko ilivyo sasa.

Misitu inajumuisha asilimia 31 (hekta bilioni 4.06) za ardhi ya dunia. Kwa sababu ya ukataji miti, idadi hii inapungua haraka. Inakadiriwa kila mwaka hekta milioni 10 za misitu hupotea, kati yake hekta milioni 3.9 iko barani Afrika.

Hivyo basi, ni jukumu la kila mmoja wetu kutilia mkazo suala la utunzaji mazingira kwa kuilinda miti iliyopo na kupanda mingine mingi mipya kwa sababu ndio mkombozi wetu katika vita ya athari za mabadiliko ya tabianchi.

Tuunge mkono kampeni za kupanda miti zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), pamoja na wadau wengine kulinda vyanzo vya miti kama vile hifadhi za misitu kwa kufichua wanaokata miti kwa makusudi.

# Bil. 3.6/- kutekeleza mradi wa Kisarawe

**Na Beatrice Shayo, KISARAWE**

ZAIDI ya Sh. bilioni 3.6 zinatarajiwa kutumika kwenye mradi wa kukusanya taarifa katika shule 30 na vituo vya afya 15 Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, mkoani Pwani kwa ajili ya kukuza uelewa wa umuhimu wa kunawa mikono kukabili magonjwa hatarishi.

Mradi huo ulioanza Oktoba mwaka huu, unatekelezwa kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Shirika la WaterAid Tanzania kwa miezi 26 hadi Novemba 2023.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo jana Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Wateraid, Anna Mzinga, alisema wanatambua usafi wa mikono na mazingira kwa ujumla ni muhimu kwa usalama wa afya za wanajamii ili kukabiliana na magonjwa yatokanayo na uchafu katika nchi na duniani kote hasa wakati huu wa UVIKO -19.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 30 ya magonjwa ya kuhara yanaweza kuzuilika kwa unawaji mikono ulio sahihi.

"Ili kuendeleza jitihadi za serikali katika kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anapata huduma za maji safi, elimu pevu ya usafi binafsi na mazingira JICA na WaterAid Tanzania wameona umuhimu wa kukusanya taarifa zitakazosaidia kukuza uelewa wa umuhimu wa unawaji mikono na usafi kwa ujumla," alisema Mzinga.

Mzinga alisema bado kuna umuhimu wa kuhamasisha unawaji hadi ifikapo 2030 ili kila Mtanzania apate huduma ya majisafi, elimu pevu ya usafi binafsi na mazingira.

Naye, Mkuu wa wilaya Kisarawe, Nickson John, maarufu kwa jina la Niki wa Pili, alisema mradi huo utahusisha utoaji elimu kwa jamii, kuhusu unawaji wa mikono, usafi wa mazingira, elimu ya usafi binafsi na utumiaji wa vyoo ili kujikinga na magonjwa ya milipuko hususan yanayotokana na uchafu. "Utafiti wa kina utafanyika ili kubaini changamoto na fursa zilizopo kupitia mradi huu. Wilayani takwimu zinaonyesha kuwa kwa kipindi cha robo mwaka Julai hadi Septemba mwaka huu, jumla ya kaya 19,075 kati ya 33,805 sawa na asilimia 57 zilitembelewa ili kutoa elimu ya afya na usafi wa mazingira, usafi binafsi na mapambano dhidi ya magonjwa ya mlipuko hasa yatokanayo na uchafu," alisema.

"Kwa upande wa vituo vya kutolea huduma za afya vyote ndani ya wilaya, bado kuna changamoto ya vyanzo vya maji vyenye uhakika. Maji hutokana na uvunaji wa mvua lakini bado kuna changamoto ya miundombinu ya uvunaji wa maji hayo," alisema.

John alisema jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya 14 kati ya 42 vina matanki na visima kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua yanayoweza kutosheleza kwa kipindi cha miezi mitatu hadi sita.

# Kampuni ya mafuta kufanya makubwa Tanzania

**Na Pascal Mayala**

KAMPUNI ya mafuta ya TotalEnergies Marketing Tanzania Limited, imeahidi kuwa itashirikiana kikamilifu na Watanzania kuijenga Tanzania bora zaidi na kufanya makubwa nchini.

Kampuni hiyo ambayo awali ilijulikana kama Total Tanzania Limited, imesema hayo baada ya kuhitimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja wake kwa mwaka 2021.

Ahadi hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Jean-Francois Schoepp, katika hafla ya kuhitimisha maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa wateja, iliyohitimishwa katika Ofisi zake Masaki jijini Dar es Salaam.

Huku akinukuu kauli ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Schoepp alisema: "Maendeleo ya kweli ni maendeleo ya watu, na sio maendeleo ya vitu, ili kupata maendeleo ya kweli ni lazima wananchi washirikishwe."

Hivyo aliahidi kwamba TotalEnergies Marketing Tanzania Limited itafanya makubwa Tanzania, kwa kuwashirikisha Watanzania, wakiwemo wateja wa TotalEnergies, katika mpango mkakati wa kampuni, na kuwataka wafanyakazi kuendelea kujituma kwa bidii hata ikibidi kufanya kazi ya ziada ili kukidhi mahitaji ya jamii kikamilifu. Katika wiki hii, wafanyakazi wa TotalEnergies Marketing Tanzania Limited wakiongozwa na Schoepp walitoa huduma kwa wateja waliotembelea vituo mbalimbali vya TotalEnergies zaidi ya 100, vilivyotapakaa nchini kote na kupata fursa ya kusikiliza maoni ya wateja, kuboresha mahusiano na wateja wao kwa nia ya kuziba mapengo yoyote yaliyopo na kujenga TotalEnergies Marketing Tanzania Limited kwa pamoja na wateja wao.

Kadhalika, wateja walipata nafasi kutoa maoni yao kuhusu huduma za Total Energies na kucheza gurudumu la bahati katika vituo hivyo na walijishindia zawadi kadhaa zikiwemo fulana, chupa za maji, kofia na bidhaa za kutunza magari.

Akiyataja miongoni mwa makubwa ambayo wanapanga kuyafanya Tanzania, Schoepp, alisema kufuatia changamoto ya upatikanaji umeme wa uhakika wamejipanga kusaidia Tanzania kufua umeme, na imejipanga kufikia mwaka 2050, itakuwa inatumia nishati jadidifu ambazo ni rafiki wa mazingira zikiwemo umemejua, umeme upepo na umeme jotoardhi.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah (wapili kulia), akikagua moja ya pikipiki za Kampuni ya Hero, wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya kwanza ya bidhaa za usafirishaji zinazotoka India, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Balozi wa India hapa nchini, Binnaya Pradhan. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wafanyabiashara waonyeshwa fursa India

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imewataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa ya maonyesho ya bidhaa za usafirishaji yaliyoandaliwa na India jijini Dar es Salaam ili kuingia ubia nayo na kukuza uchumi.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maonyesho ya bidhaa za usafirishaji ambazo zinaingizwa nchini kutoka India.

Akizungumza katika ufunguzi wa maonyesho hayo yaliyoandaliwa na Ubalozi wa India nchini, alisema ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania.

"Hizi kampuni ambazo zinaonyesha bidhaa zake hapa hasa za uchukuzi kuanzia pikipiki, bajaji, magari na matrekta, zana hizi ni muhimu katika kukuza uchumi, jitihada hizi zinapelekea namna kampuni hizi zinaunga mkono dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan, anayetaka nchi iende kwenye uchumi wa viwanda," alisema.

Dk. Abdallah alimpongeza balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Pradhan, kwa kuandaa maonyesho hayo kwa kuwa yanatoa fursa kwa Watanzania kwenda kutafuta fursa katika biashara za ubia.

"Huwezi kuwa na biashara endapo huna zana bora za kilimo, tumeshuhudia kampuni za matrekta zipo hapa na wanayatoa kwa mikopo, huwezi kuwa na biashara nzuri kama huwezi kusafirisha mazao, tumeshuhudia kampuni za kusafirisha mazao na mizigo.

"Hata sekta ya biashara ndogo pikipiki na bajaji nazo zipo ambazo nazo zinatolewa kwa mkopo kwa wanaozihitaji, ubalozi umefanya jambo kubwa," alisema.

Dk. Abdallah alisema ubalozi huo umemhakikishia kuwa viwanda vya bidhaa hizo ambazo kwa sasa zinaletwa kutoka nje na kuunganishwa hapa baadae watazizalisha Tanzania.

Balozi Pradhan alisema wameandaa maonyesho hayo ya vifaa vya usafirishaji vinavyotoka nchini kwao ili kuuza.

"Tunashirikiana na taasisi za fedha za India na za Tanzania kuwawezesha wateja watakaotaka kununua bidhaa hizi. Kampuni hizi za India zimewekeza dola za Marekani milioni 150 hapa Tanzania na shabaha yao siyo kuuza tu, kampuni hizi zimetengeneza ajira kwa Watanzania," alisema.

# Wahitimu UDSM waja na mfumo kukabili madalali

**Na Romana Mallya**

WAHITIMU wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), katika kukabiliana na tozo kubwa za madalali wanaojishughulisha na upangishaji nyumba na uuzaji wa viwanja wamebuni mfumo wa kidigitali unaowakutanisha moja kwa moja wamiliki na wateja.

Mshauri wa masuala ya kisheria, Hamza Jabir, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mfumo huo mpya wa kidigitali unaojulikana kama SETO.

"Mfumo huu unalenga kuleta suluhisho la tatizo ambalo Watanzania wamekuwa wakikumbana nalo wanapotaka nyumba za kupanga, viwanja, hoteli wakati wa sikukuu au mikutano, kupitia mfumo huu mteja anayetaka nyumba badala ya kumlipa dalali kodi ya mwezi mmoja, atatoa Sh. 10,000 tu," alisema.


Pia alisema mfumo huo utatoa ajira kwa vijana kwa sababu watakaoweka nyumba na zikachukuliwa watajiingizia kipato cha Sh. 6,000.

"Mfano mtu akiweka kwenye ukurasa wetu nyumba 10 na watu wakazihitaji maana yake atakuwa amejiingizia kipato kikubwa kwa siku," alisema.

Mwanzilishi mwenza na Mkurugenzi wa kampuni, Frank Mwandi, alisema baada ya kumaliza chuo UDSM walipata shida ya upangaji wa nyumba kwa sababu walikuwa hawana fedha ya kulipa tozo za madalali ndiyo maana wakaamua kuja na mfumo huo.

"Tuliwaza kwa sababu tumeanzisha kampuni ya kutengeneza software, kwa nini tusitengeneze mfumo wa kusaidia tatizo hili, hivyo mwaka 2019 tulitengeneza mfumo wa SETO ambapo tuliiwasilisha UDSM na walitupongeza na kututaka tupokee maoni ya watu ili kuboresha zaidi," alisema.

Alisema baada ya kufanya utafiti walibaini watu wengi wana uhitaji wa nyumba za kupanga na viwanja, lakini wakati mwingine wanakutana na tatizo la tozo mbalimbali za madalali.




Meneja Mawasiliano wa Vodacom Tanzania, Christina Murimi (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa kongamano la Data Tamasha 2021 litakaloanza Jumatatu ijayo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kampasi ya Kijitonyama (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano - CoICT), lenye lengo la kujadili umuhimu wa data kwenye uchumi wa kidijitali. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Data Lab (dLab), Stephen Chacha na Mwakilishi wa Mwananchi Communications Ltd, Mihayo Wilmore. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya madai kughushi cheti cha ndoa yakwama

**Na Kulwa Mzee**

SHAURI la kughushi cheti cha ndoa na cheti cha kuzaliwa cha mtoto limekwama kuendelea kusikilizwa, jalada liko kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) likisubiriwa maelekezo.

Shauri hilo lipo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu katika hatua ya kusikiliza mashahidi mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Ritha Tarimo.

Mshtakiwa katika kesi hiyo ni Khairoon Jandu, upelelezi ulishakamilika na mashahidi upande wa Jamhuri walishaandaliwa.

Wakili wa upande wa utetezi, Abubakar Salim, Novemba 29, mwaka huu, alidai mbele ya Hakimu Tarimo kuwa shauri linasubiri maelekezo ya DPP.

Baada ya Wakili Abubakar kueleza hayo, Hakimu Tarimo aliiahirisha kesi hiyo mpaka Desemba 29, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa ili kuangalia kama jalada la kesi limerejea.

Kesi hiyo awali ilikuwa inasikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Joseph Lwambano ambaye amekuwa msajili, sasa itaendelea kusikilizwa na Hakimu Tarimo.

Mashahidi ambao walishaandaliwa kutoa ushahidi ni Wakili Jerome Msemwa na Sheikh wa BAKWATA, lakini ilishindikana kuendelea kusikilizwa kwa ushahidi wa mashahidi hao wa Jamhuri baada ya DPP kuliitisha jalada la kesi hiyo. Mashahidi wengine ambao walishapewa hati ya wito ili waweze kutoa ushahidi katika kesi hiyo kwa upande wa mashtaka ni kutoka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita), Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Polisi na Hospitali ya Hindu Mandali.

Kwa upande wa mashtaka kesi hiyo inaendeshwa na Wakili wa Serikali Ashura Mnzava.

Katika shtaka la kwanza, inadaiwa katika tarehe na mwezi usiojulikana mwaka 2020 jijini Dar es Salaam, mshtakiwa kwa njia ya udanganyifu alighushi cheti cha kuzaliwa cha mtoto, Gurditsing Jandu akionyesha kuwa kimetolewa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (Rita) wakati akijua kuwa ni uongo.

Katika shtaka la pili, mwaka 2020 mshtakiwa alighushi cheti cha ndoa akionyesha kimetolewa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) jambo alilojua kuwa sio kweli.

# 2% tu wenye VVU mkoa Kagera wachanja corona

**Na Lilian Lugakingira,** KARAGWE

ASILIMIA mbili ya watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU) katika Mkoa wa Kagera ndiyo wamepatiwa chanjo ya ugonjwa wa Uviko-19.

Hali hiyo ilitokana na uwapo wa mwitikio mdogo kwa kundi hilo, ambalo linatajwa kuwa miongoni mwa makundi yaliyoko katika hatari ya kupata maambukizi ya ugonjwa huo.

Akizungumza katika maadhimisho ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kimkoa katika wilaya ya Karagwe, Meneja Miradi wa Shirika lisilo la kiserikali ambalo linahudumia watu wanaoishi na VVU katika Mkoa wa Kagera (MDH), Dk. Laizer Isack alisema kuwa mkoa wa Kagera una watu wanaoishi na VVU zaidi ya 85,000, lakini waliojitokeza kuchanjwa ni asilimia mbili pekee.

Meneja huyo wa MDH ambao pia wanashirikiana na serikali kuhamasisha wananchi hasa wanaosumbuliwa na magonjwa sugu kupata chanjo ya Uviko-19.

Alisema ili kuhakikisha watu hao wanapatiwa chanjo hiyo na kuongeza kinga katika mwili, wameweka vituo vya kutolea chanjo katika kliniki za tiba na matunzo kwa watu wanaoishi na VVU, ili watakapofika wasisumbuke kwenda sehemu nyingine.

"Bado mwitikio kwa kundi hili upo chini sana ikilinganishwa na makundi mengine ya watu wasio na VVU, kwa hiyo tunajitahidi kuhamasisha kupitia katika kliniki za tiba na matunzo, ili watakapofika waweze kupatiwa chanjo pale pale," alisema Dk. Isack.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Watu wanaoishi na VVU katika Wilaya ya Karagwe, Saada Abdalah, aliwataka watu wanaoishi na virusi vya ugonjwa huo, kufika vituoni kupata chanjo kutokana na miili yao kuwa na upungufu wa kinga, hivyo ni rahisi wao kushambuliwa na magonjwa kama UVIKO-19.

Akisoma taarifa katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii katika Wilaya ya Karagwe, Edna Kyabyazi, alisema kuwa katika upimaji uliofanyika kupitia vituo vya tiba mwaka 2020, hali ya maambukizi mapya katika Mkoa wa Kagera ilikuwa asilimia 4.1 na kwamba katika kipindi cha miezi tisa ya mwaka 2021, yamepungua na kufikia asilimia tatu.

"Kitengo cha afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kimekuwa kikiendelea kupambana na janga la Ukimwi, ikiwamo kuweka mikakati ya kuibua ambao hawajaweza kupima na kujua afya zao, hasa kwa njia ya upimaji wa njia ya mshirika wa ngono na kufanikiwa kupunguza maambukizi, jitihada hizi ni endelevu lengo likiwa ni kuhakikisha yanapungua zaidi," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, aliwataka wananchi kuepuka visababishi vyote vinavyochangia kuwapo kwa maambukizi mapya ya VVU, ikiwamo ulevi wa kupindukia, matumizi ya dawa za kulevya, ngono zembe na biashara ya ngono.

## HABARI KITAIFA

# Shirika lasambazia vijana mamilioni kondomu miaka 5

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la T-MARC Tanzania, limeuza na kusambaza kondomu milioni 60 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, kwa watu wa rika mbalimbali, walengwa wakiwa ni vijana na watu walio katika sehemu hatarishi.

T-MARC pia imekuwa ikitoa mafunzo ya kuhamasisha matumizi ya kondomu za Dume Classic, Dume Desire, na Dume Extreme, ambazo pia watu wananunua kulingana na uwezo wao wa kipato.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa T-MARC Tanzania, Oliveria Tarimo, siku moja baada ya maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani, yaliyofanyika kitaifa jijiji Mbeya, mgeni rasmi akiwa ni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

"T-MARC Tanzania ina jukumu ya kuhakikisha jamii inapata huduma za afya za kudumu na za uhakika kwa kushirikiana na washirika wake, na imekuwa ikifanya hivyo karibu miaka 20 iliyopita," alisema Tarimo.

Alifafanua kuwa, kabla ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, shirika hilo, lilishiriki kwenye maonyesho, yaliyoandaliwa kwa ajili ya maadhimisho hayo na kutoa mafunzo ya kuhamasisha matumizi ya kondomu.

"Maonyesho hayo yalifanyika jijini Mbeya, nasi kama mshirika wa karibu wa serikali ya Tanzania katika vita vya mapambano dhidi ya Ukimwi, tulionyesha na kutoa mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo," alisema.

Alisema, shirika pia limeelimisha umma katika huduma za afya kuhusu mapambano dhidi ya kifua kikuu, uzazi wa mpango, afya ya uzazi, lishe, malaria, maji na suala la usafi wa mazingira pamoja na kuhamasisha utoaji wa nafasi kwa mtoto wa kike katika maendeleo yake.

"Mmesikia takwimu kwamba, maambukizi mapya VVU kwa vijana yako juu, nasi T-MARC tumetoa na tunaendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha matumizi ya kondomu zao pendwa za Dume Classic, Dume Desire, na Dume Extreme, ili kuwakinga Watanzania wakiwamo vijana," alisema.

Akihutubia katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Ajira, Uratibu wa Bunge, Vijana na Watu Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema maambukizi yanaongezeka.

Katika ufafanuzi wake alisema, maambukizi mapya kwa vijana kati ya miaka 15 hadi 24 yamezidi kuongezeka huku wasichana wakiwa vinara katika hatari zaidi kukumbwa na janga hilo.

Kwa mujibu wa waziri huyo, taarifa za utafiti zinaonyesha kuwa maambukizi mapya ya VVU yanawakabili zaidi vijana wenye umri huo, na kwamba yamefikia asilimia 40 huku asilimia 80 kati ya hao wakiwa ni wa kike.

Aidha, aliitaja mikoa ambayo maambukizi yako juu ya kiwango cha kitaifa kuwa ni Njombe, Iringa, Mbeya, Kagera na Geita, huku mikoa ya Geita, Simiyu, Manyara na Dodoma nayo ikiwa na kasi kubwa ya maambukizi.

# Katibu Mkuu ataka weledi wa madaktari

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Tixon Nzunda, amewataka madaktari kuzingatia weledi na maadili wanapofanya tathmini za ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi.

Nzunda aliyasema hayo jijini Mbeya, wakati akifungua mafunzo ya siku tano ya tathmini za ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi kwa madaktari na watoa huduma za afya wapatao 100 kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Katavi, Rukwa, Songwe, Mbeya, Ruvuma, Njombe na Iringa.

"Wakati wote mnapaswa kuzingatia misingi mitatu wakati mkitekeleza majukumu yenu, weledi, uadilifu na uwajibikaji," alisema Nzunda.

Alisema kosa lolote dogo litakalofanywa katika kazi ya kufanya tathmini ya ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi litapelekea athari katika maisha ya watu, uchumi wa nchi na kuhujumu mfuko," alisema Nzunda. Aidha, alisema lengo la serikali la kuanzisha mfuko wa fidia kwa wafanyakazi ni kuhakikisha wafanyakazi wanapata mafao bora tofauti na sheria ya zamani ya fidia kwa wafanyakazi ili kuboresha fidia.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, alisema katika kuhakikisha mfuko unafanya jukumu lake kubwa la kutoa fidia kwa wale ambao wanapatwa na majanga kutokana na kazi, mfuko unazingatia kufanya tathmini kwa usahihi na kwa haraka.

"Hili la usahihi lina maanisha tunahitaji kushirikiana na wenzetu hawa ambao tayari ni wataalamu katika maeneo hayo na hili la uharaka lina maanisha mfuko hauwezi kuwa na madaktari kila kona ya nchi kwa hiyo tunahitaji madaktari ambao wako kwenye vituo mbalimbali ili kushirikiana nasi katika kuhakikisha suala la tathmini linafanywa kwa haraka, hivyo muhusika anapata fidia stahiki na kwa wakati." Dk. Mduma.

Alisema mfuko utaendelea kufanya kazi zake kwa weledi ndiyo maana unaendelea kuwajengea uwezo wataalamu hao wa afya.

"Kuna miongozo ili kuhakikisha tathmini zinazotolewa na wataalamu hawa zinakuwa na uhakika, zinaaminika na zinatabirika kwa maana kwamba ziko consistent pale ambapo ukifanyiwa tathmini na mtaalamu A na B matokeo yasitofautiane," alifafanua.

Dk. Mduma aliishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu na Serikali kwa ujumla kwa jinsi ambavyo imekuwa ikishirikiana na mfuko katika kuhakikisha unaendelea kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akimkabidhi cheti na ngao Makamu wa Rais wa Kampuni ya GGML, Simon Shayo (kushoto), kwa kutambua mchango wa kampuni hiyo katika mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi. Wanaoshuhudia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama (katikati) na Mkurugenzi wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko. GGML imekabidhiwa cheti hicho jana jijini Mbeya katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yamwaga mil. 84/- za mapambano ya VVU/ Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imechangia zaidi ya Sh. milioni 84 kusaidia mipango ya serikali katika mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Mbeya.

GGML na Tume ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) kupitia kampeni ya Kilimanjaro Challenge, wanashirikiana kwa namna mbalimbali ikiwamo kuongeza uelewa kuhusu janga la VVU na Ukimwi ili siku moja Tanzania itangazwe kuwa imetokomeza kabisa janga hilo katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani juzi jijini Mbeya, Makamu wa Rais wa GGML anayeshughulikia miradi endelevu, Simon Shayo, alisema kaulimbiu ya mwaka huu isemayo "Zingatia Usawa, Tokomeza Ukimwi, Tokomeza magonjwa ya mlipuko," ni muhimu kwa jamii ya Geita na Tanzania kwa ujumla.

Alisema mpango wa GGML Kili Challenge ni mradi mahsusi kutoka katika sekta binafsi ambao umeisaidia serikali kwa zaidi ya miaka 20 katika mapambano dhidi ya VVU.

"Kupitia mpango huu, wachangiaji wenzetu wameendelea kuwa mstari wa mbele kudhibiti janga la VVU kwa kuhakikisha utoaji huduma za kimatibabu unazingatia utu na haki za wale wote wanaoweka imani yao kwetu hususani wale walio hatarini zaidi.

"Tunaziomba sekta binafsi nchini kuungana na GGML na kusaidia mfuko wa Ukimwi ili kuwezesha mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi kuwa endelevu. Bila kuwa na mipango imara ya kuhakikisha usawa katika utoaji wa huduma hizi za kimatibabu ni dhahiri dunia itashindwa kufikia lengo lake la kutokomeza Ukimwi ifikapo mwaka 2030," alisema.

Shayo aliongeza kuwa maendeleo chanya ya kijamii na kiuchumi ya mkoa na Tanzania ni matokeo ya jamii yenye afya.

# Wasichana wapewa siri kusoma masomo sayansi

**Na Zainab Kihate,** BAGAMOYO

WANAFUNZI wa kike nchini wametakiwa kukimbilia masomo ya sayansi, ili kutengeneza madaktari wengi wa kike ili kuweka uwiano sawa na madaktari wa kiume.

Hayo yamesemwa na Mbunge wa Bagamoyo, Muharami Mkenge, alipokuwa akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Zamzam inayofundisha masomo ya sayansi, iliyoko kata ya Yombo wilayani Bagamoyo mkoani Pwani.

"Tunahitaji mama zetu wanapokuwa na matatizo mbalimbali hasa ya faragha basi wakienda hospitali wasiwe wanyonge, wakutane na kinamama wenzao ili wawe huru kujieleza matatizo yao," alisema.

Naye Mkurugenzi wa shule hiyo, Yahya Msonde, akizungumza katika mahafali hayo alisema kuwa maumivu ya faragha za kike kushughulikiwa na madaktari wa kiume sio tu zinawaumiza kinamama wenyewe bali, hata wanaume zao wanaumizwa na hali hiyo.

"Sisi kinababa tunajikaza tu, lakini hakuna baba anayependa kuona mkewe ana faragha za kike anatibiwa na dokta mwanaume, ikiwemo kuzalishwa na dokta mwanaume," alisema.

Mkurugenzi huyo alitoa wito kwa wadau wa elimu nchini, kujenga shule zenye mtazamo kama wa Zamzam, ili wasichana wengi nchini wapate nafasi ya kusomea sayansi na kupata madaktari wengi wa kike.




Meneja Uhusiano wa Benki ya Biashara ya DCB, Fauzia Bairu (kulia), akimsikiliza Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa Mfuko wa Mitaji ya Maendeleo ( UNCDF), Peter Malika wakati wa kongamano la wadau kuhusu utaratibu mbadala wa kugharamia miradi ya maendeleo ya kiuchumi kwa kutumia hati fungani, lililoandaliwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mitaji (UNCDF), jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# W/biashara waiangukia serikali sheria za kodi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA mkoani Njombe wameiomba serikali kuandaa muswada wa marekebisho ya sera na sheria za tozo za kodi ambazo zimekuwa kandamizi kwao, jambo ambalo linakwamisha jitihada za kuinua uchumi na pato la taifa.

Ombi hilo walilitoa kwa Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Msafiri Mbibo, alipozungumza na wafanyabiashara mbalimbali wa mkoani Njombe katika kikao maalum cha kusikiliza kero na changamoto zao.

Akizungumza katika kikao hicho, mwenyekiti wa wafanyabiashara Halmashauri ya Mji wa Njombe, Eliud Pangamawe, alisema changamoto ni sera na sheria za kikodi ambazo baadhi yake utekelezaji wake ni mgumu.

"Nadhani ipo haja ya kuzifanyia marekebisho kupitia ushauri wenu kwa viongozi wa ngazi ya juu ambao mnafanya nao kazi kwa sababu zimekaa katika mfumo ambao kidogo utekelezaji wake ni mgumu kwa mfano, kodi ya VAT sasa hivi hapa Njombe sisi wakulima wa mbao tunazozwa kodi ya VAT kwenye mbao na wafanyabiashara wengi wanataka tafsiri ya sheria hii vizuri ili waweze kutimiza wajibu wao katika kuisimamia, kuitekeleza hii sheria ambayo imewekwa," alisema Pangamawe.

Awali akizungumza na wafanyabiashara hao, Mbibo ambaye aliongozana na Naibu Kamishna wa Kodi za Ndani, Swalehe Byarugaba, alisema ni wajibu kwa wafanyabishara kujenga utamaduni wa kulipa kodi ili kusaidia nchi kukuza uchumi ikiwamo kuimarisha miundombinu mbalimbali.

"Kodi ni uchumi na maendeleo, uchumi ni ustawi na uthabiti, kodi ni ustawi na uthabiti, tunapokuwa tukiona maendeleo mbalimbali ya vitu mbalimbali, huduma za maji, umeme wa uhakika na huduma mbalimbali tunazozipata huo ni ustawi," alisema Mbibo.

Mbibo aliongeza kuwa ili huduma ziweze kupatikana ni lazima kodi iwepo.

Kwa upande wake, Byarugaba alisema tangu serikali ilipohimiza wafanyabiashara kuzingatia kuuza bidhaa kwa kutoa risiti bado mwitikio ni mdogo.

"Bado kuna wafanyabiashara wale wachache ambao sio waaminifu, aidha lisiti haitoki anakwambia mashine mbovu au risiti inatoka kwa kiwango cha chini ili mradi risiti isitoke sasa hapo ndio panapoleta shida," alisema Byarugaba.

# Samia kufungua kiwanda cha nyaya za mawasiliano

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

RAIS Samia Suluhu Hassan anatarajia kufanya ziara ya siku moja katika Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, pamoja na mambo mengine kuzindua kiwanda.

Akizungumzia na waandishi wa habari kuhusiana na ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, alisema ziara hiyo ambayo itafanyika, mbali ya kuzungumza na wananchi, atazindua kiwanda cha kutengeneza nyaya za mawasiliano (Fiber optics) kilichoko Mkuranga.

Kunenge alisema Rais anatarajia kuzungumza na wananchi wa Vikindu na baadaye kuzindua kiwanda hicho ambacho ni kikubwa Afrika kwa kutengeneza nyaya za mawasiliano.

"Hii ni heshima kubwa kwetu kuwa na kiwanda kikubwa kama hiki ambacho ni kati ya viwanda vikubwa." Niwapongeze hapa Afrika, kingine kikiwa ni Afrika Kusini, Algeria na Misri, niwaalike wananchi tujitokeze kwa wingi kwenye maeneo ambayo Rais atapita," alisema.

Kunenge alisema serikali inaendelea kuboresha mazingira ili mkoa huo ambao unaongoza kwa viwanda wawekezaji waendelee kuongezeka.

Aidha, alisema katika msimu wa korosho ulioanza Novemba, korosho zaidi ya tani 11.9 zimeuzwa kati ya hizo daraja la kwanza ni asilimia 77.2.

Kunenge alisema tofauti na msimu wa mwaka jana daraja la kwanza iliuzwa kwa Sh. 1,300 mwaka huu katika minada ambayo imeshafanyika zimeuzwa kwa Sh. 2,040, hatua ambayo ni ya mafanikio.

Akizungumzia suala la kilimo, Kunenge aliwapongeza wakulima wa korosho kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu ambao waliwapatia kwenye mikutano ya wadau na kuwatembelea kwenye maeneo yao.

"Wakulima kwa kuwa na mabadiliko hasa katika haya mazao ya kimkakati jitihada zetu zimeanza kuonyesha matunda kwa pamoja tutaleta mabadiliko ya kiuchumi," alisema.

Kunenge pia alisema mabadiliko hayo pia yamechangiwa na uboreshaji wa huduma za kiugani, uvunaji na upatikanaji wa masoko hali ambayo inaleta matarajio ya kuwa na korosho bora zaidi kwa mwaka 2022, ambazo zitafungua masoko ya ndani na nje ya mkoa huo.



Ukurasa 12

KILELE SIKU YA WENYE ULEMAVU

Mwenye ulemavu kijana 'asiyejiweza' asimulia alivyoweza kutoka nyumba ya nyasi, hadi bati



KILELE SIKU YA WENYE ULEMAVU

**Wahusika waorodhesha mapengo walio nayo katika kunufaika na haki za umma**

Ukurasa 14



LICHA KUZIDISHIWA LENGO…

# NFRA Songea yanunua mahindi 'mpaka basi' shida sasa hifadhi

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

SONGEA imo katika mikoa nane ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula cha Taifa (NFRA) nchini, majukumu ya wakala huyo ni pamoja na kununua na kuhifadhi chakula (mahindi).

Jukumu kubwa la wakala huo katika kununua nafaka, pia chanzo cha mapato kwa halmashauri zote zilizopo mkoani Ruvuma, zikilipa ushuru wa mazao. Pia imekuwa ikitoa ajira ya muda kati ya vijana 300 hadi 600.

Serikali kupitia NFRA imeendelea kununua mahindi ambayo kwa mwaka iliipa Kanda ya Songea kununua jumla ya tani 41,000 za mahindi, kiwango ambacho kimeongezeka ikilinganishwa na msimu uliopita 2020/2021. Ni nyongeza ya asilimia 25.

Meneja wa NFRA Songea, Morgan Mwaipyana, anazitaja changamoto anazokutana nazo katika ununuzi wa mahindi kutoka kwa wakulima, inajumuisha ufinyu wa maghala. Inatajwa kuwa tatizo kubwa, pamoja na wakala kufanikiwa kununua mahindi ya wakulima, bado wanakabiliwa na tatizo la upungufu wa maghala.

Anasema kutokana na serikali kuwaongezea kiwango cha ununuzi wa mahindi, kumekuwapo ugumu wa kupata maghala hasa vijijini, ambako ndiko ununuzi unafanyika, hivyo wanalazimika kuhifadhi nje, jambo ambalo siyo salama, kwa sababu ya hali ya hewa iliyopo.

Mwaipyana anafafanua zaidi kuwa, wakati msimu wa mvua ndio unakaribia, anahofu mahindi yanaweza kuingia katika hatari ya kunyeshewa, kama hatua za haraka hazitachukuliwa.



Ghala la kuhifadhia mahindi la Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) Kanda ya Songea. **PICHA: GIDEON MWAKANOSYA**

Anasema, hadi sasa wameshanunua mahindi tani zaidi ya Tani 26,000 ambayo ni sawa na wastani wa asilimia 63. 4 au theluthi mbili za lengo tajwa na wanaendelea kununua mahindi hayo kutoka kwa wakulima.

"Tayari serikali imeshatoa kiasi cha Sh. bilioni 13 kwa ajili ya malipo ya tani 21,000 za mahindi ya wakulima na tayari zimeshalipwa na zoezi linaendelea," anasema Mwaipyana.

Meneja hiyo anasema, kwa sasa kuna maghala sita ya kuhifadhi nafaka yanatofautiana uwezo wa kuhifadhi, kati ya tani 4000 hadi 8000 kwa wakati mmoja, lakini kukidhi hitaji kunahitajika msadaa wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 za mahindi yaliyoongezeka, kwani wamekwama pa kuweka zaida.

Akifafanua, anasema maghala yaliyopo vijijini, mengi uwezo wake ni tani 300 hadi 500, hivyo wanalazimika kukodi ili uhifadhi mahindi wanayonunua. Hata hivyo, wanaendelea kutafuta maghala makubwa zaidi, ambayo yatasaidia kuhifadhi mahindi hayo.

Pia Meneja Mwaipyana anawashauri wafanyabiashara kuona umuhimu wa kutafuta masoko mengine, badala ya kutegemea kuuza mahindi yao NFRA pekee, kwani hawawezi kununua mahindi yote ya wakulima.

Mwaipyana anataja ugumu mwingine unaochelewesha kazi zao, ni ununuzi wa mahindi kutoka kwa wakulima kuwa ni pamoja na uhaba mkubwa wa vifungashio. Hapo anaiomba serikali ichukue hatua za haraka kutatua shida hiyo.

Anasema ili kumaliza ugumu wanahitaji vifungashio 820,000 vinavyoletwa kwa awamu, jambo linalochangia kuwapo kero ya upatikanaji vifungashio vya kuwekewa mahindi, ambayo tayari yameshanunuliwa kutoka kwa wakulima.

**RC RUVUMA**

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, anasema mradi wa kununua mahindi unaotekelezwa na NFRA katika Kanda ya Songea, unajenga vihenge vya kisasa (silos) 12 vyenye uwezo wa kuhifadhi nafaka tani 45,000.

Pia kuna jumla ya maghala mawili yenye jumla ya tani10,000 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 10.16 sawa na shilingi bilioni 23.37 na iliyokuwa inajengwa na inatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba 2020.

Anasema kukamilika kwa mradi huo utafanya Kanda ya Songea, una uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 84,000 ndani ya maghala na vihenge kwa wakati mmoja, pamoja na vihenge hivyo vya kisasa.

Mkuu wa Mkoa anasema mradi unajenga miundombinu wezeshi kama stoo ya vifaa, viuatilifu, ujenzi wa ofisi, maabara, vyoo, kantini, uzio na barabara za ndani.

KILELE SIKU YA WENYE ULEMAVU

# Mwenye ulemavu kijana 'asiyejiweza' asimulia alivyoweza kutoka nyumba ya nyasi, hadi bati

- Msaada mbuzi watatu 'wamtoa' kumiliki miradi
- Leo 'pedeshee' kijijini, dira mpya hoteli ghorofa
- Naibu Waziri 'ampa tano' akitumia mfano binafsi

**Na Romana Mallya**



Nyumba ya Zengo Tobangaba, ikiwa ni sehemu ya mafanikio yake. **PICHA ZOTE: ROMANA MALLYA**

UNAPOINGIA Kijiji cha Busongo Kata ya Mwamashele wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, kwenye orodha ya wajasiriamali wake hakosekani Zengo Tobangaba, mwenye umri wa miaka 25.

Huyo ni kijana mwenye ulemavu wa miguu (kuanzia kwenye nyonga), lakini hilo halijawa sababu asijishughulishe na miradi ya maendeleo.

Akiwa na umri huo mdogo wa miongo miwili na nusu, tayari anafurahia mafanikio ya mradi wake wa ufugaji mbuzi na ng'ombe na ameanzisha mingine ambayo ni kilimo cha pamba na banda la kuangalia mipira, ili kujiingizia kipato.

Ilikuwaje? Tobangaba anasimulia safari ya maisha yake kuwa alizaliwa akiwa hana ulemavu wowote. Alibahatika kusoma mpaka darasa la nne, ndipo akalazimika kuacha shule.

"Sikuweza kuendelea, kwa sababu nilikuwa sijui kusoma, hivyo miaka 12 iliyopita niliacha shule na sababu kubwa ni kwa kuwa nilikuwa sijui kusoma," anasimulia, akiwa mtoto wa tano kati ya saba kwenye uzaliwa wao nyumbani.

**ULEMAVU ULIPOMFIKA**

Tobangaba, anasema baada ya hapo alibaki nyumbani kwa miaka. Ilipotimu umri wa miaka 15 wakati huo akipendelea zaidi kucheza mpira, alianza kuhisi anaishiwa ngumu kwenye viungo vyake mwilini.

"Nilianza kusikia baadhi ya viungo vyangu vinaishiwa nguvu, ninapata ganzi mara kwa mara na kidogo kidogo vikaanza kubadilika baada ya mama kuhangaika sana nimeishia kuwa ulemavu," anasimulia.

Anasema, licha ya ulemavu alioupata hakuwahi kukata tamaa au kuvunjika moyo asifikie malengo yake aliyojiwekea.

Tobangaba anasimulia mwaka 2015 akiwa kijijini kwao, alikutana na shirika lijulikanalo kama Tanganyika Christian Refugee Service (TCRS) linalojishughulisha na kuwasaidia vijana, ambalo lilimpatia mbuzi watatu, kati yake wawili majike.

Anasimulia aliwatunza mpaka idadi yao wakaongezeka kufikia 40, ndipo akaanza kuwauza na wangine wanabaki kuzaliana. Anaendelea:

"Kila nilipouza, nilikuwa ninahifadhi fedha zikitosha kununua bati, nikawa nanunua moja moja mpaka yakafikia mabati 10. Nikawaomba vijana wa kijiji kwetu wakanifyatulia matofali, nikanunua misumari na mbao nikaanza ujenzi wa nyumba ya vyumba viwili."

Kijana huyo anasema alianza ujenzi kwa hatua na ndani ya muda mfupi akamaliza na sasa anaishi kwenye makazi hayo, akihama kutoka nyumba ya matope iliyokuwa imeezekwa kwa majani.

"Sasa ninajivunia kuishi kwenye nyumba ya kisasa ya bati nimeijenga kwa gharama ya zaidi ya shilingi 250,000," anatamka, akiwa miongoni mwa vijana wanne waliobahatika kuhudhuria katika kongamano la kitaifa la kuzungumzia ukatili wa kijinsia kwa wenye ulemavu Jumanne ya wiki hii, jijini Dar es Salaam.

Akiwa na mengi anayosimulia mbele ya Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Wenye Ulemavu, Ummy Nderiananga, kwa bashasha kubwa usoni, anatamka:"Mbuzi watatu niliopewa na TCRS wameniwezesha kujenga nyumba ya bati, nilikuwa naishi kwenye nyumba ya tope, juu ikiezekwa na nyasi."

Anataja siri ya mafanikio hayo ni malengo aliyojiwekea awatunze waongezeke na baadaye auze ili atoke kwenye nyumba ya nyasi na kuingia kwenye iliyoezekwa kwa bati.

Baada ya mafanikio hayo ya makazi, anasema akaingia katika lengo lingine hata akajenga kibanda anachouzia bidhaa ndogo, sasa amenunua ungo na runinga anakoonyesha mpira ambako watu wanaingia kwa kiingilio Sh. 200 kila mmoja.

"Banda hili kama kuna mipira mingi kwa mwezi sikosi Sh. 100,000. Ninamshukuru Mungu. Binafsi ni shabiki wa timu ya Simba," kauli hiyo ikafanya mashabiki wenzake ndani ya kongamano hilo kushangilia, huku akiendelea kwa kibwagizo, "Lakini Yanga ni watani wangu," kicheko kikatawala.

Tobangaba anasimulia kuwa miradi hiyo miwili imefungulia fursa nyingine, kwani sasa analima zao la pamba kwenye shamba lenye ukubwa wa ekari tatu na mavuno yake yanampatia hadi Sh. 400,000.

"Nisisahau, nilinunua ng'ombe, nimempeleka kwa jirani ninamkodisha kwa kilimo, nao ni mradi mwingine ambao ninajivunia kuwa nao," anasimulia.

Ilikuwa hadhira ya kongamano hilo lililoandaliwa na

na Shirika la Wanawake katika Sheria ya Maendeleo Afrika (WiLDAF), ikiwa ni sehemu ya kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati dhidi ya Ukatili wa Kijinsia (UWAKI).

Kijana huyo anawashangaza washiriki, anapoeleza ndoto yake ya kumiliki hoteli ya ghorofa atakayoijenga, huku akihitimisha kwa kuwashauri vijana wenzake waache kukaa vijiweni na kusema hawana ajira.

"Unakuta mtu amesoma bado analalamika hana ajira, kwa nini usijiajiri? Vijana muache kukaa tu, mjishughulishe, mkalime na mkivuna baada ya kuuuza msile fedha yote, mtunze fedha kidogo mnayoipata, siku moja itaongezeka na mtafanya maendeleo makubwa zaidi kuliko niliyoyafanya," anasema.

**WAFADHILI WA TCRS**

Kiongozi wa Mradi TCRS wilayani Kishapu, Oscar Rutenge, anasema shirika lao ndio mfadhili wa mradi wa Finnish Evangelical Lutheran Mission (FELM), Finland, ikiwalenga wenye ulemavu.

"Mradi wetu ulianza mwaka 2012 na mwaka mmoja mbele 2013 tulifanya utafiti wa kuwatambua wenye ulemavu wilayani Kishapu, kwa kupita nyumba kwa nyumba.

"Zengo Tobangaba, alikuwa miongoni mwa walemavu 331 tuliowafikia. Miongoni mwao, wapo watoto, vijana, watu wazima na wazee wenye ulemavu tofauti," anafafanua.

Anasema walipomfikia Zengo mwaka 2015, walimkuta anaishi na mama yake mzazi na ndugu, lakini kutokana na hali ya ulemavu wake, alikuwa mtu wa kubaki nyumbani wakati wote, wakati familia ikienda shambani kulima.

"Alitueleza wakati mwingine alikuwa anakosa hata chakula kwa sababu ndugu zake walikuwa wakishinda shambani. Alitueleza hali hiyo ilikuwa inamkatisha tamaa kama mwenye ulemavu.

"Kwa sababu lengo la shirika ni kumwezesha mlemavu ajimudu mwenyewe, baada ya kumwelimisha pamoja na mama yake, Zengo alituomba tumpatie mbuzi.

"Ndipo tukampa watatu kama alivyoeleza, wakazaliana na kufika 40. Mbuzi wakafungua na miradi yake mingine, anajitahidi, hakuchagua kukata tamaa kuwa hawezi kwa sababu ya ulemavu," anaeleza.



Kijana Zengo Tobangaba, akiwa kwenye duka lake ambako pia anaendesha huduma ya ufundi wa elektroniki, vilevile anaonyesha michezo ya soka kwa kiingilio maalum.

**WAZIRI WA MFANO**

Ni kauli inayoungwa mkono na Naibu Waziri Ummy Nderiananga, ambaye ana ulemavu wa miguu, anaiambia kongamano la wenye ulemavu, akitaja sehemu ya mambo yanayowakatisha tamaa wanawake, wasichana na vijana wenye ulemavu.

Anarejea dhana 'siwezi' hakukubaliana nayo, hata hatua aliyofikia sasa anakuwa shuhuda wa mafanikio, akisisitiza "(mwenye ulemavu), akienda huku anaambiwa 'huwezi', akirudi huku anaambiwa 'huwezi'. Sasa niwaambie, mnao uwezo mkubwa, msikatishwe tamaa na mtu yeyote, songeni mbele mtafika mbali.

"Hata wanawake wenzangu wenye ulemavu waliopo hapa mjini (Dar es Salaam), wapo wanaowakatisha tamaa sasa waliopo kijijini? Hali si inazidi kuwa mbaya wenzangu?

"Kwa hiyo msikatishwe tamaa, tena mliopo hapa mliopata fursa hii ya uelewa mkubwa kuhusu ukatili wa kijinsia kwa vijana, watoto, wanawake wenye ulemavu, tembeeni kifua mbele endeleeni kujiamini.

"Nyie wenyewe msijibague wala kujinyanyapaa, kwa sababu kuna kunyanyapaliwa na watu na kujinyanyapaa mwenyewe, namna unavyojichukulia mbele za watu, yaani watasema 'siwezi', usijinyanyapae."

Naibu Waziri huyo anawapa mbinu ya kufika mbali, ni lazima wapambane kwa kujiamini, umma nao umwamini, akitumikia mfano binafsi: "Mimi ninajiamini au sijiamini? Mimi tena si unaona! ...Kusema kweli ninajiamini, ndiyo maana ninawahimiza kwa sababu nimejiamini.

"Hapa nilipo panahitaji kujiamini, usipojiamini hata hoja yako inaweza kuwekwa pembeni, ukijiamini inakurahisisishia. Hata kama una masuala yako unataka kufanya, watu watasema huyu anajiamini kwenye jambo fulani," anawapa darasa hadhira iliyomshuhudia.

Pia anasisitiza jumuiya hiyo anayoilenga iendelee kupendana, kusaidiana na wakikoseana wasameheane ili wasonge mbele, akiwapa elimu ya picha kuhusu uhalisi wa mageuzi yanayoendelea:

"Mheshimiwa Rais wakati anawaapisha makatibu wakuu Ikulu, watu mitandaoni walikuwa wanaandika, heeh! Rais kamteua hadi huyu mwenye ulemavu? Mtu mwenye ulemavu kashikiwa magongo yake anaapa, kwa hiyo zipo hatua zinaendelea kupigwa.

"Wakati zinapigwa hapa nchini, Afrika, duniani, mjiamini, sisi tukiweka mipango vizuri ya kisera halafu msipojiamini, tutapishana," anawaeleza kwa kujivunia kuwa na Rais mwanamke, akibashiri hata uwezekano wa kuwa na Rais mwenye ulemavu upo.

"Akitokea huyo mtu muwe tayari kuchukua nafasi nyinyi wanawake, wasichana na vijana wenye ulemavu. Vijana wenye ulemavu endeleeni kusoma kwa bidii, tupo pamoja na nyie tunawaunga mkono," anawaeleza.

Pia anawakumbusha katika Sensa ya Watu na Makazi inayotarajia kufanyika mwakani, walemavu wasijifungie ndani, wajitokeze kufanikisha.

**UJUMBE WA KANISA**

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheli Tanzania (KKKT), Askofu Fredrick Shoo, anasema mjadala katika kongamano hilo ni muhimu kwa sababu unahusu kutambua haki ya kuishi bila ukatili kwa wanawake na vijana wenye ulemavu.

"Tupo hapa kuwaomba wote ambao wameshiriki katika kuwatendea ukatili wa aina yoyote wenye ulemavu kwamba waache, wabadilike na vilevile watubu, kuna haja ya kweli ya toba pale ambapo tumewaonea kwa sababu zozote zile tupo hapa kuweka uwazi," anasema.

Mkurugenzi Mtendaji wa WiLDAF, Anna Kulaya, anasema kongamano hilo linatoa fursa ya uzinduzi wa mradi mpya wa 'Chaguo langu, Haki yangu' chini ya Shirika la Idadi ya Watu Ulimwenguni (UNFPA) ambao unafadhiliwa na serikali ya Finland na unatekelezwa na WiLDAF, ukiwa na thamani ya Dola za Marekani milioni sita.

Pia anakumbusha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa wakati akizindua Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, aliwataka waandalie sera, mifumo na sheria zenye mapungufu kisha wajadiliane na mapendekezo yawasilishwe serikalini kwa hatua zaidi.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA nchini, Jacqueline Mahon, anauelezea mradi mpya wa 'Chaguo langu Haki yangu' kuwa ni wa miaka mitatu na nusu ambao lengo ni kuhakikisha haki za wenye ulemavu wakiwamo wanawake na wasichana zinalindwa na kuimarishwa kupitia hatua za pamoja zinazopambana na ukatili wa kijinsia na mila potofu.

Anataja takwimu za sensa ya mwaka 2012 iliyofanyika nchini na kueleza kuwa, zinakadiria kuwa asilimia 9.3 ya watu wa Tanzania wanaishi na ulemavu, ingawa hazijajumuisha vijana au watoto kwenye kundi hilo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watanzania tusijiaminishe kuwa Uviko-19 umetuzoea!






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

WATANZANIA tuendelee kusalimiana kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huku tukizingatia hatari tunayoiona kuhusu ugonjwa wetu huu, ambao sasa tunaanza kuuzoe kijinga wa UVIKO-19.

Ugonjwa huu baada ya kukaa kwa heshima kama alivyopata kusema mmoja wa waliopata kuwa viongozi wa chama cha siasa nchini, hivi sasa kirusi chake kimejibadilisha na kuja kivingine.

Wanasema wataalamu, kirusi hicho kimeonekana Kusini mwa Bara hili la Afrika, kinaitwa Umicron, kwamba hivi sasa hiki ni kijanja ile mbaya, kina uwezo wa kukwepa hata chanjo dhidi yake, hivyo kutahadharishwa kuwa tujiweke sawa.

Lakini, tukiangalia na kutazamana, tunaonekana Watanzania kama hatujali vile, yanaingilia sikio hili na kutokea lingine. Tunataka mpaka tuone tunaangamia ndipo tukae mkao sawa wa kujiepusha na hili.

Ni bahati mbaya kwamba tuna historia hiyo ya kudharau mambo na kujifanya tunajua kuliko wengine. Tunakuwa wabishi kwa kila jambo, tunaambiwa kuna korona tunasema ikae kwa heshima.

Tunaambiwa chanjo ni muhimu tunabisha, kwamba haina uhakika kwa sababu chanjo hii utafiti wake haukuchukua muda mrefu mpaka kutumika. Tunaunda kamati ya kumshauri Chifu Hangaya ambaye anakubaliana na matokeo ya uchunguzi.

Lakini, bado tunabishana kushinikiza kuwa mkichanja msipokufa baada ya miaka miwili basi mtageuka mazombi. Na wasemao hayo ni viongozi wa makundi makubwa tu yanayoheshimika na kuamini wana ushawishi.

Haya sasa Umicron keshafika Kusini mwa Afrika, tuseme Kusini mwa Janga la Sahara, tunafanyaje sasa? Hatukwepi kwa sababu nchi hii ina pakanana nchi za Kusini mwa Afrika.

Viongozi wetu chini ya Chifu Hangaya wanashinikiza kila siku kujiepusha na maambukizi ya ugonjwa huu hatari, lakini tunaonekana kama hatusikii vile na tunapuyanga tuna mambo yetu.

Hivi nani anavaa barakoa kama awali? Nani leo ananawa maji tiririka na sabuni kama ilivyokuwa awali katika kila mlango tukishuhudia ndoo za maji na sabuni?

Nani hivi sasa anaogopa mikusanyiko? Hakuna, ndiyo kwanza tunafurika misibani, maharusini, michezoni, ngomani na katika matamasha ya siyo miguu wala kichwa?

Tunakanyaga na kwenye daladala na mwendokasi kama siafu, hakuna anayejua wala kujali kuwa kuna ugonjwa unaitwa UVIKO-19. Tatizo letu Watanzania mpaka tusikie kiongozi fulani kafa kwa UVIKO-19 ndipo tushtuke.

Utadhani tumeshikiwa akili na watu fulani na hatujijali wenyewe wala familia zetu. Tunaacha watoto wanajichunga kama nyumbu porini. Tunakwenda kokote na tunaingia mahali popote bila kujali kama kuna gonjwa.

Juzi Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya akaja na mwongozo wa namna ya kuepuka na maambukizi ya ugonjwa huu mpya, ikiwa ni pamoja na 'level seat' kwenye daladala zetu hizi.

Akasema hata kuona mgonjwa hospitali wasizidi watu wawili. Hivi nani katika muktadha huu atasimamia mambo haya? Najiuliza nakosa jibu la papo kwa hapo, kwa sababu najua Watanzania tulivyo wabishi.

Tukawa kama mazezeta tusio jifikiria kila tukiona kiongozi haja vaa barakoa, nasi hata kama tulivaa tunavua, ili kumfurahisha badala ya kujali maisha yetu.

Tukumbuke, maisha si mali ya serikali, maisha si mali ya viongozi, maisha ni mali yetu wenyewe na Mungu wetu. Kila mtu aamini kuwa yuko salama kwa kujilinda na si kwa kusubiri kulindwa kama mbuzi. Uviko ipo, iepukwe na chanjoni pale pale, usipotaka hujitaki.

Tuelewe hata kama chanjo ni hiyari, lakini maambukizi si hiyari. Tukatae kuambukiza na hata kuambukizana na tukitaka kazi iendelee, lazima nasi tuendelee kuchanja. Umicron ni hatari kuliko tunavyodhani. Alamsiki!

## KILELE SIKU YA WENYE ULEMAVU

# Wahusika waorodhesha mapengo walio nayo katika kunufaika na haki za umma

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KILA inapotimu Desemba 3 ya mwaka dunia huadhimisha Siku ya Watu Wenye Ulemavu, mwaka huu ikiwa na ujumbe "uongozi na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu kuelekea ujumuishwaji na ufikiwaji endelevu baada ya Uviko-19."

Tayari kunatajwa kuwapo baadhi ya wanajamii wanaoamini kuegemea matendo yasiyo sahihi, badala ya kuwahurumia jamii ya watoto kwa baadhi ya kasoro walizo nazo, hata wakatendewa mema.

Wakati dunia inaadhimisha siku hiyo ya watu wenye ulemavu, kuna sura ya pili inakabiliwa na janga la maradhi ya Uviko-19. Hapo inaibua maswali, je, wenye ulemavu hao wamefikiwa kikamilifu, hata wakapatiwa elimu sahihi ya kujikinga na ugonjwa huo?

WAHUSIKA WANAONGEA

Saada Hamad, Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar, anasema licha ya serikali kuelimisha jamii, bado kuna kundi kubwa la kada hiyo haijafikiwa kupatiwa elimu ya kukabili maradhi ya corona hasa ikizingatiwa ni ugonjwa usiochagua mtu.

Anasema, kutokana na uhaba wa wakalimani wa lugha ya alama Zanzibar, wenye ulemavu wa uziwi ndio kundi kubwa lililoachwa nyuma katika kupatiwa elimu hiyo stahiki.

"Wanahitaji kufikiwa zaidi, kwa sababu wakalimani waliopo ni wachache, hivyo huchelewa kupata uelewa wa jambo lolote lile sio tu elimu ya corona," anasema Saada.

Pia anafafanua kwamba bado kuna kundi kubwa la wenye ulemavu, hawajapata chanjo husika ya corona, ili kujikinga na ugonjwa huo, akiwa na maoni ni vyema wakafikiwa na kupewa elimu kuhusu umuhimu wa chanjo husika.

Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu, Injinia Ussi Khamis Dedes, anasema elimu inatolewa kuhusu kujikinga na corona ili wenye ulemavu wafikiwe, lakini shida iliyoko kwa watu wenye uziwi, kutokana na uhaba wa wakalimani.

Anafafanua kwamba wenye ulemavu kupitia jumuiya zao, wamepatiwa visaidizi vya kujikinga na Uviko-19, ikiwamo kupatiwa vitakasa mikono na barakoa.

Injinia Dedes anawataka wenye ulemavu, waendelee kuchukua tahadhari za kujikinga na ugonjwa husika, uliokwishapoteza maisha ya wengi duniani.



Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Fatma Abdulhabib Ferej (kushoto), alipokabidhiwa vifaa kwa ajili ya wenye ulemavu, kutoka kwa Msimamizi wa Jumuiya ya Wazanzibar wanaoishi nchini Canada, Bishara Al Masroori. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Anasema hakuna utafiti uliofanywa wa kujua kiwango cha ajira kwa watu wenye ulemavu walioajiriwa, lakini wapo baadhi ya vijana wenye ulemavu wameajiriwa serikalini.

Mdau mwingine ni Idrisa Daima, kutoka Idara ya Watu Wenye Ulemavu, anasema uzoefu unaonyesha vikwazo vya mawasiliano vinawaathiri zaidi wenye ulemavu.

Anakiri kuna vikwazo vya mtazamo hasi vinavyochangia kwa kiwango kikubwa kuibua vikwazo vingine akitoa mfano wa baadhi ya wenye ulemavu kupata ugumu pale wanapotaka kwenda sehemu nyingine.

Daima anafafanua kuwapo itikadi potofu zinazozua ugumu katika upatikanaji wa maisha mazuri kwa wenye ulemavu, hata wakajikuta wanaangukia ugumu wa maisha, pia umaskini uliokithiri.

Unyanyapaa, ubaguzi na kutengwa ndani ya jamii, ni mtazamo hasi unaotajwa kuzaliwa na mitazamo ya duniani kuhusu hali ya ulemavu kwa binadamu.

### FURSA ZA AJIRA

Sura nyingine inayolalamikiwa kwa upande wa Zanzibar inagusa ufinyu fursa za ajira kwa wenye ulemavu, haiko katika kiwango cha kuridhisha, ikilinganishwa wasio na kasoro hizo Visiwani.

Abdulkadir Amin Ahmed, ana ulemavu wa kuona. Anataja namna wanavyopata ugumu wa kuajiriwa kwa wasio na ulemavu, licha ya kwamba wana sifa stahiki za kuajiriwa.

Mwenye ulemavu huyo anasema, bado baadhi ya waajiri hawaamini wenye ulemavu katika kuwapatia ajira, ilhali wana uwezo stahiki wa kufanya kazi kama watu wenzao wasio na ulemavu.

"Ulemavu tulio nao isiwe kikwazo cha kutopata fursa ikiwamo ya ajira na sisi, tuna familia tunahitaji kupata ajira ili kuendesha familia zetu," anasema.

Salma Sadat, Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, anasema hakuna utafiti uliofanywa kujua kiwango cha ajira kwa wenye hali hiyo walioajiriwa, lakini anakiri kuwapo waajiriwa serikalini.

Anarejea hadi sasa hawajaridhika na kiwango kilichoko cha walioajiriwa wakati kuna kundi kubwa la wenye ulemavu wasio na ajira, wakati baadhi yao wana sifa stahiki.

Sadat anasema kuna hitaji la juhudi za makusudi kuwapatia ajira wenye ulemavu katika taasisi mbalimbali, ili kupunguza wimbi lao wasio na ajira, akiwasifu ni wachapa bora, hivyo ni vyema kuwazesha kielimu ili wawe na ujuzi unaohitajika.

Anasema pasipokuwapo elimu, kutaishia kuwa tatizo kwa wenye ulemavu, hivyo anashauri jamii kuacha kuwaficha watu wenye ulemavu na badala yake kuwapeleka shule.

Pia anawataka walimu kuwa karibu na watoto hao kitaaluma, ikiwa ni sehemu ya mchango wao kwa jamii hiyo.

Mratibu wa Jumuiya ya Wenye Ulemavu Wasioona Zanzibar, Adil Muhammed, anasema watu hao wana changamoto ya ajira, hasa kwa wenye ulemavu wa akili, ndio wameachwa nyuma zaidi, hivyo ajira zinahitajika kwa kuwa bado wana haki za kibinadamu na kimaisha kama jamii nyinginezo.

### KUTOKA KWA WAZIRI

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, anasema katika kuimarisha na kusimamia fursa na haki za wenye ulemavu, ofisi yake kupitia Idara ya Watu Wenye Ulemavu, imefanya mapitio ya awali ya sheria inayowahusu wenye ulemavu ya mwaka 2006, hivyo sasa rasimu husika inaendelea kupata maoni ya wadau.

Anasema marekebisho ya sheria hiyo yataongeza ufanisi katika utoaji haki na fursa kwa wenye ulemavu, pamoja na kuimarisha sekta mbalimbali zinazogusa maisha yao, hali anayosema itawaboreshea maisha.

"Ili kuhamasisha uelewa juu ya haki na fursa za watu wenye ulemavu, ofisi yangu inashirikiana na taasisi zisizo za kiserikali 10 kuhamasisha marekebisho ya miundombinu ya majengo, hususan ya serikali kwa ajili ya kufikika kwa urahisi zaidi," anafafanua.

Pia anataja miundombinu ya majengo na barabara inayoendelea kurekebishwa, imewasaidia kwa kiasi kikubwa wenye ulemavu na kuwaepusha kutoka vihatarishi vilivyokuwapo awali.

Waziri huyo anasema, kuna magumu ya baadhi ya watu wenye ulemavu kushindwa kupata matibabu, kwa sababu ya kutomudu gharama za matibabu na uhaba wa dawa hospitalini kwa wenye ulemavu mchanganyiko.

Zanzibar inakisiwa kuwa na jumla ya wenye ulemavu 74,500, hata hivyo idadi ya waliosajiliwa kidigitali na Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu, umefanikiwa kusajili watu 8,488, katika mgawanyo wanawake 4,043 na wanaume 4,445.

Ushauri wake ni kwamba, ulazima uliopo ni kuitaka jamii iamke kuhakikisha haki za wenye ulemavu zinapatikana, kwa sababu kutopatikana kwake, kunazidisha ama kuduma au kuzorota maendeleo ya wenye ulemavu na taifa kwa ujumla.

Ili haki hizo kupatikana jamii hiyo iwe chanya, kuna ushauri hatua za makusudi ziwepo ikijumuisha hata huruma kwa kundi hilo, kwa mustakabali unaoegemea ustawi wa jamii waliko.




Kiongozi wa Jumuiya ya Wanawake wenye Ulemavu Zanzibar akizungumza.





## Waziri: SIDO ongezeni majengo ya wajasiriamali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amelitaka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kuongeza majengo yatakayosaidia wajasiriamali kuzalisha bila kutumia mitaji mikubwa.

Kigahe alisema hayo wakati wa ziara ya kutembelea viwanda vya wajasiriamali wadogo na wa kati.

Akiwa katika eneo la uwekezaji wa viwanda la SIDO Kizota alitaka shirika hilo kuwekeza kwenye majengo kwani bado kuna wahitaji wa maeneo ya viwanda.

"Eneo hili bado ni kubwa mnaweza kujenga majengo zaidi na kuwapa fursa wajasiriamali kufanya uzalishaji katika maeneo salama na bila kunitajia mitaji mikubwa," alisema.

Pia alisema moja ya changamoto ya bidhaa za Tanzania ni kutokuwa shindani na zile zinazotoka nje ya nchi ikiwamo za ngozi.

Alisema kinachotakiwa ni kuhakikisha kunakuwa na viwanda vingi zaidi na hata vivyozalisha soli za viatu ili kupunguza utegemezi wa kuagiza nje ya nchi.

Aidha, aliitaka SIDO kuendelea kuwasimamia wajasiriamali wenye viwanda ili waweze kutimiza malengo yako kwenye kuuza mitaji na masoko.

Mkurugenzi Mkuu wa SIDO, Mhandisi Prof. Sylvester Mpanduji, alisema shirika hilo limekuwa likisimamia maeneo manne ikiwamo bidhaa za teknolojia, kutoa huduma ya ujenzi wa miundombinu, kutoa mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na mrefu, masoko, kuandaa maonyesho ya kanda, kitaifa.

Aidha, kutoa mikopo kupitia Mfuko wa NEDF ulioanzishwa mwaka 1994.

Kaimu Meneja wa SIDO, Mkoa wa Dodoma, Justine Kahemela, alisema fursa zilizopo mkoani hapa ni uwepo wa malighafi ya kilimo cha zabibu, alizeti na karanga.

Pia uwepo wa madini kama dhahabu, gypsum, uwepo wa ardhi ya kutosha miundombinu bora kama vile barabara, maji umeme na uwapo wa njia za kuunganisha nchi jirani pande zote.

Alisema wapangaji waliopo katika mtaa mdogo wa viwanda ni 32 katika sekta ya chuma, mbao, magari, mamalishe, uchapishaji na wauza vipuri ambapo jumla ya ajira zilizotolewa ni 228 za kudumu na za muda 140.

"Na thamani ya uwekezaji waliofanya wajasiriamali ni Sh. milioni 293 wastani wa mauzo yao kwa mwezi Sh. milioni 52.25 na wastani kwa mwaka ni Sh. milioni 639.04.

Aidha, alisema kituo cha mafunzo ya bidhaa za ngozi kimefunguliwa mwaka 2000 ambapo mpaka sasa kozi 84 kwa wajasiriamali 1,680 zimetolewa ambao baadhi yao wameanzisha viwanda.

# Kasi mimba za utotoni Chamwino yatisha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATI ya wajawazito 14,900 waliojifungua katika kipindi ya mwaka 2020 wilayani Chamwino mkoani Dodoma 3,438 ni wasichana waliokuwa katika umri wa chini ya miaka 18.

Aidha, katika kipindi hicho wasichana waliojifungua katika umri wa chini ya miaka 20 kati yao 359 walikuwa wamefanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia vya ukeketaji.

Takwimu hizo zilitolewa jana na Mratibu wa huduma za afya ya uzazi na watoto wilaya ya Chamwino, Neema Mlula, wakati alipokuwa akizungumza na wakazi wa kijiji cha Iringa Mvumi kwenye maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsi katika wilaya hiyo bado vipo kwa wingi hali ambayo inahitaji jitihada za makusudi kuvikabili.

"Ukatili mwingi unafanyika nyumbani wanafamilia ndiyo tunakuwa wakwanza kulindana watoto wetu wanalawitiwa katika nyumba zetu lakini tunaogopa kusema kwa kuona aibu," alisema.

Kadhalika, alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo bado vimeshika kasi katika wilaya hiyo ni mimba za utotoni na ndoa katika umri mdogo.

Alisema, watoto wengi wapata ujauzito katika umri mdogo na kushindwa kumaliza masomo yao lakini watuhumiwa hawachukuliwi hatua kutokana na kulindana.

"Mimi kama nilivyosema hapo awali ni mratibu wa masuala ya afya ya uzazi na watoto hivyo nafahamu katika wilaya yetu namna ambavyo hali ilivyo wasichana wengi wanakuja kujifungua wakiwa na umri wa chini ya miaka 18, lakini wengine tayari wameshaolewa katika umri kama huo na kuacha masomo," alisisitiza.

Naye mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Shida Hamisi, alisema moja ya sababu ambazo zinachangia kuongezeka kwa ndoa nyingi za utotoni ni viongozi wa dini kushiriki katika kufungisha ndoa bila kuhoji umri wa wanandoa.

"Kuna ndoa moja tulishuhudia sitataja kanisa kuna binti alikuwa anaoelewa kimwonekano tuu anaonyesha ni mtoto mdogo anaolewa na baba mtu mzima lakini mchungaji wala hakuhoji na kuendelea kufungisha ndoa ile," alisema.

Kutokana na hali hiyo aliwaomba viongozi wa dini kuhakikisha kuwa kila wanapofungisha ndoa wapate vyeti vya kuzaliwa vya wanandoa.

Ofisa kutoka Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Florence Chaki, alitoa wito kwa wakazi wa kijiji hicho kujitokeza kutoa malalamiko yao pindi wanapoona haki yao inapotea.

"Tume milango yake ipo wazi kama mnaona kunashida ambayo inasababisha kupoteza haki yenu njooni msikae kimya nakusema tuu namwachia Mungu pambaneni kupata haki yenu na sisi tutawasaidia," alisema Chaki.

Maadhimisho hayo ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Jinsia yanafanyika katika wilaya hiyo kwa kuratibiwa na Shirika la Action Aid Tanzania.



Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri (kushoto), akipimwa afya yake na Ofisa Muuguzi wa Jiji la Dodoma, Josephine Mkude, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, yaliyofanyika kiwilaya katika Kata ya Nzunguni, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Maofisa mipango wasisitizwa usimamizi mipango maendeleo

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MAOFISA mipango nchini wametakiwa kuhakikisha kuwa wanapanga na kusimamia vyema utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa kuweka na kutekeleza vipaumbele vya taifa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Aldof Ndunguru, alitoa rai hiyo wakati wa kufungua kongamano la wanamipango la mwaka 2021 lililofanyika ijini hapa.

Ndunguru, aliwataka kuhakikisha kuwa wanapanga vema mipango ya maendeleo kwa kutekeleza na kuweka vipaumbele vya taifa vilivyokusudiwa.

"Mtakubaliana nami kuwa taifa letu linakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ukosefu wa ajira kwa vijana, athari za mabadiliko ya tabianchi, umaskini na maradhi ya Uviko hivyo wanamipango tunalojukumu la kusimamia vizuri utekelezaji wa mipango iliyowekwa na seikali," alisema.

Aidha, alibainisha kuwa wanajukumu kubwa la kupanga na kusimamia pamoja na kutatua matatizo yaliyopo kwenye maeneo yao ya kazi ili kuleta tija.

Aidha, alitoa rai kwa wanampango kuendelea kutoa ushauri na mapendekezo kwa serikali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya kimsingi kwenye maeneo yao ya kazi.

Ndunguru alisema wizara yao ipo pamoja na wanamipango wote nchini na itayafanyia kazi maoni na mapendekezo yenye nia njema yatakayotokana na mkutano mkuu huo wa mwaka.

Kwa upande wake Kaimu Kamishna Idara ya Mipango ya Kitaifa Wizara ya Fedha na Mipango, Ekingo Magembe, alisema kongamano litafanyika kwa siku tatu na dhima yake ni mwanamipango imara kwa ustawi wa taifa.

Magembe alisema dhima hiyo imetokana na nia ya dhati ya serikali ya kuendeleza na kuwezesha wanamipango kuongeza maarifa na weledi katika utendaji kazi wao.

Alisema washiriki wa kongamano hilo ni wachumi, maofisa mipango, watakwimu na wanademografia kutoka wizara mbalimbali, idara zinazojitegemea na wakala wa serikali.

Aliwataja wanamipango wengine wanaoshiriki katika kongamano hilo kuwa kutoka taasisi na mashirika ya umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa sababu wanahusika katika uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji na kutathmini mipango ya kisekta ya taifa.

Hata hivyo, alisema lengo la kongamano hilo ni kuwajengea uwezo wanamipango hao katika namna bora ya uchambuzi wa sera pamoja na kujadili dira ya taifa ya maendeleo ya mwaka 2025.



# Majaliwa asisitiza wasichana waliopata mimba kurudi shule

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amepigilia msumari mabinti wote waliokatiza masomo kwa sababu ya ujauzito, kurudi shuleni kuendelea na masomo ili kutimiza ndoto zao.

Majaliwa aliyasema hayo juzi, wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya Ukimwi duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya.

Waziri Mkuu, alisema serikali imeandaa mazingira wezeshi kwa ajili ya mabinti walioachishwa masomo kutokana na ujauzito, kurejea masomoni.

"Serikali yenu sikivu ilichakata jambo hilo la mabinti wanaoachishwa masomo kutokana na ujauzito kutokana na mazingira mbalimbali wanayokutana nayo, sasa wanarudi shule kuendelea na masomo," alisema Majaliwa.

Alisema sababu ya kufanya hivyo ni baada ya kubaini wengi wao wanapata ujauzito kutokana na sababu ya hali ya maisha na kurubuniwa hivyo kupitia waraka wa elimu, wanayosifa ya kuendelea kusoma.

Awali katika hotuba yake Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), Leticia Mouris alieleza kuwa mabinti wengine waliopata maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), pia walipewa ujauzito.

Aliishukuru serikali kwa kuwaruhusu mabinti waliojifungua kurudi shule na kwamba hatua hiyo itasaidia wao kusoma kwa bidii na kutumiza malengo yao ya baadae kupitia elimu.

"Baraza letu lina mabinti ambao licha ya kuwa na maambukizi ya VVU, pia wana watoto ambao asilimia kubwa wanawalea kwenye mazingira magumu nafurahi serikali imeliona hili na kutoa maelekezo kwa wizara ya elimu kwa sasa warudi shule," alisema Leticia.

Leticia, aliiomba serikali kuhakikisha inaweka mazingira rafiki ya upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya ugonjwa wa UKIMWI, kwa makundi ya watu wenye ulemavu na wajawazito.

Alisema kutokana na uhaba wa miundombinu rafiki, ikiwamo barabara, kwa kuwa wagonjwa katika kundi hilo wanashindwa kumeza dawa kwa wakati kutokana na kutembea umbali mrefu kuzifuata.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na watumishi wa Chuo cha Biashara (CBE) Kampasi ya Mbeya, wakati wa uzinduzi wa ujenzi wa chuo hicho kinachojengwa Kata ya Iganzo, jijini Mbeya mapema wiki hii. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Marekani yaahidi wadau ushirikiano

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI ya Marekani imesema itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo redio za kijamii katika mapambano dhidi ya Ukimwi ili kufikia lengo la taifa la kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Balozi wa Marekani, Dk. Donald Wright, alitoa kauli hiyo alipotembelea kituo cha Radio Highlands Fm, kilichopo eneo la Jakaranda jijini Mbeya ikiwa ni maadhimisho ya kilele cha siku ya Ukimwi duniani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya.

Balozi Donald alisema kuwa Marekani inatekeleza programu mbalimbali nchini Tanzania zinazolenga masuala ya afya ukiwemo Ugonjwa wa ukimwi na kwamba katika utekelezaji wake wanashirikiana na wadau.

"Marekani itaendelea kushirikiana na serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, katika masuala mbalimbali ikiwemo mapambano dhidi ya Virusi vya Ukimwi, ndio maana hata leo mmetuona kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya Ukimwi duniani," alisema

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kituo cha Redio cha Highland fm, Jacqueline Mwakyambiki alimshukuru balozi Dk. Donald kwa kufanya ziara katika kituo hicho na kueleza kuwa hali hiyo inadhihirisha jinsi redio hiyo ilivyokuwa mnufaika kwa serikali ya Marekani kupitia programu mbalimbali.

Akizungumzia mchango wa vyombo vya kijamii katika mapambano dhidi ya Virusi Vya Ukimwi Jacqueline alisema jamii ina imani na vyombo vya habari, hivyo nafasi yake katika kufikia dira ya serikali ya kutokomeza VVU, ifikapo mwaka 2030 ni kubwa.

"Asilimia zaidi ya 90 ya wananchi wanasikiliza redio, hivyo ni rahisi kuwafikia kwa kutoa elimu na kuhamasisha umma kujikinga dhidi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi".

# Wanahabari wahitimu mafunzo ya uongozi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAANDISHI wa habari wanawake 12 kutoka Tanzania, wamehitimu mafunzo ya uongozi yanayoendeshwa na Taasisi ya Kimataifa ya WAN- IFRA/ Women in News kutoka nchi saba barani Afrika.

Mafunzo hayo yaliyoendeshwa kwa kipindi cha miezi tisa yamehusisha wanahabari wanawake kutoka nchi za Rwanda, Zimbabwe, Uganda, Kenya, Zambia, Malawi na Botswana .

Akizungumza juzi wakati wa halfa ya kuwatunuku vyeti vya kuhitimu mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa WAN- IFRA/ Women in News, Melanie Walker alisema mwaka huu umekuwa wa vikwazo vingi duniani na sekta ya habari ni miongoni mwa iliyokumbana nazo kutokana na janga la corona.

"Tunatambua kuwa kila mmoja wenu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, amekuwa akikabiliwa na matatizo mengi yakiwamo ya kifedha, kiusalama, kitaaluma na kiafya, hivyo kutokuwa na uhakika wa nini cha kufanya, ili kuimarisha ustawi wake kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19, ambao umesababisha umasikini kwa wananchi na kuchangia vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwenye jamii," alisema Walker.

Alisema licha ya vikwazo hivyo, mwaka 2021 umekuwa na mafanikio makubwa katika njanya mbalimbali ukilinganisha na miaka mingine na kwamba jumla ya wahitimu 92 waliochaguliwa kushiriki 91 wamehitimu mafunzo hayo. Mkurugenzi Afrika, Women in News, Jane Godia alisema mafunzo hayo, huwajengea uwezo wanahabari wanawake pamoja na wahariri katika masuala mbalimbali kama vile uongozi wa taasisi za habari, uandishi wa habari za takwimu, mitandaoni, usimamizi wa fedha, maadili ya uanahabari, kupambana na unyanyasaji wa kijinsia hususan katika mtandao.

Mwakilishi wa SIDA, Fredrick Westerholm, ambaye pia ni mwakilishi mfawidhi wa program wa masuala ya demokrasia, haki na uhuru wa kujieleza, alisema kazi zinazofanywa na Women in News za kuwajengea uwezo wanahabari wanawake zinachochea usawa na kuunga mkono jitihada za serikali ya Sweden, kulinda na kutetea masuala ya haki za binadamu na uhuru wa kutoa maoni.

Miongoni mwa wanahabari Watanzania waliohitimu mafunzo hayo ni Grace Mwakalinga kutoka kampuni ya The Guardian Limited, Oliver Nyeriga kutoka runinga East Africa Television (EATV).



## Wizara, JKCI kutibu wagonjwa wa moyo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imetia saini mkataba wa makubaliano na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI)kupeleka wagonjwa wa moyo wanaotoka Zanzibar.

Mkataba huo ulisainiwa jana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo,Fatma Mrisho na Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Prof. Mohammed Janabi.

Akizungumza baada ya utiaji saini huo, Katibu Mkuu Mrisho alisema mkataba huo una manufaa makubwa kwa wanachi na utawasaidia katika kupatiwa matibabu kwa gharama nafuu.

Alisema uwepo wa taasisi hiyo nchini umeiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutumia gharama nafuu katika matibabu ya moyo, ikilinganishwa na kupeleka wagonjwa nje ya nchi jambo ambalo husababisha gharama kubwa kwa serikali.

Aidha alisema serikali inaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha gharama zinazohitajika zinalipwa ili wananchi kupatiwa matibabu katika taasisi hiyo.

Kwa upande wake, Prof. Janabi, alisema jumla ya wagonjwa 200 kutoka Zanzibar walipelekwa katika taasisi hiyo kwa ajili ya matibabu, kati yake 31 walifanyiwa upasuaji na kupatiwa matibabu na hakuna aliyepoteza maisha.

Alisema uamuzi wa serikali ya Zanzibar wa kupeleka wagonjwa katika taasisi hiyo, umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za kifedha ikilinganishwa na kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

Alieleza taasisi hiyo ina mpango wa kuwaleta wataalamu wake Zanzibar ili kuwafanyia uchunguzi wa awali wagonjwa wa moyo kabla ya kusafirishwa kwa ajili ya matibabu.

Aidha, alisema JKCI ipo tayari kuendeleza ushirikiano na hospitali ya rufaa ya Mnazi mmoja, ili kuhakisha wananchi wanapata matibabu nchini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Dk. Marijani Msafiri, alisema ipo haja ya kuweka miundombinu ya kuwa na Taasisi ya Moyo Zanzibar ili wagonjwa kupata matibabu visiwani hapa.

Pia, bado ushirikiano wa karibu unahitajika baina ya hospitali ya rufaa Mnazi mmoja na JKCI ili wagonjwa wa moyo kupata matibabu kwa wepesi.

# Rais Mwinyi asisitiza uchumi imara Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali anayoiongoza ina lengo la kuhakikisha inajenga uchumi imara utakaoleta maendeleo kwa wananchi wote.

Rais Dk. Mwinyi aliyasema hayo hivi karibuni alipokutana na kufanya mazungumzo na viongozi na wajumbe wa Baraza la Wazee wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Ofisi Kuu ya CCM, Kisiwandui Zanzibar, waliokwenda Ikulu Jijini Zanzibar kumpongeza.

Alisema siasa ni uchumi na ikiwa nzuri, uchumi huimarika, na kwamba juhudi za makusudi zinaendelea kuchukuliwa na serikali kuhakikisha kunajengwa uchumi ulio imara na madhubuti.

Aidha aliwaeleza wazee hao mipango na mikakati ya serikali kuimarisha sekta za maendeleo ikiwa ni pamoja na vijana kupata ajira na serikali nayo kupata mapato.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, jambo la msingi ni kuhakikisha Zanzibar inaendelea kupata maendeleo na kuujenga uchumi imara ni kuwepo kwa amani na utulivu, juhudi ambazo zimechukuliwa katika kuhakikisha hilo linafanyika.

Pia, Dk. Mwinyi alitumia fursa hiyo kulipongeza baraza hilo kwa kuendeleza utamaduni wao wa kukutana na kiongozi aliyeko madarakani kwa azma ya kuzungumza na kubadilishana mawazo.

Alisema serikali itahakikisha jengo la kihistoria la Beit al Jaib linajengwa upya na kurudi katika hadhi yake ya asili ujenzi ambao unatarajiwa kuanza rasmi hapo Febuari mwakani.

Pia, kuimarisha huduma za afya kwa kuanzisha huduma za bima ya afya ili kurahisisha kila mwananchi kupata matibabu kirahisi.

Awali katika tamko lao lililosomwa kwa niaba yao na Mzee Haji Machano, walieleza kufurahishwa na kazi iliyofanyika ikiwamo ziara kwenye wilaya kukagua shughuli za maendeleo na wananchi kueleza kero zao.

"Umekemea rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma, umerekebisha mfumo mzima wa elimu na kukarabati utawala, umekemea ubakaji, udhalilishaji wa watoto na wanawake, umechukizwa sana na uingizaji na utumiaji dawa za kulevya nchini na umeunda chombo cha udhibiti na ufuatiliaji, umepanua uchumi wa bluu na kuiweka Wizara maalum ya shughuli hizo, umewaita wawekezaji," alisema.

Aidha, baraza hilo lilishauri kujengwa nyumba ya ASP, iliyopo jangwani ambayo ina historia kubwa pia, walishauri kujengwa kwa jengo la Bait el Jaib, kuongeza kasi ya kupiga vita vitendo vya ukatili, ubakaji, udhalilishaji wa watoto na wanawake, uingizwaji wa dawa za kulevya pamoja na kupambana na maradhi ya mlipuko.

Wakati huo huo, Rais Dk. Mwinyi alikutana na wawekezaji wa kampuni ya Sukari Kilombero wakiongozwa na Balozi Ami Ramadhan Mpungwe waliopo visiwani humo kwa mkutano na aliwapongeza kwa mipango mizuri ya upanuzi wa kiwanda hicho.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud, akiwaaga wananchi baada ya kuhutubia maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, katika viwanja vya Kidimni, wilaya ya Kati Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman ataja sababu vikwazo huduma kwa wanaoishi na VVU

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kukosekana usawa katika upatikanaji huduma kwa watu wanaoishi na VVU kunachangia kuendelea kuwepo kwa ugonjwa wa Ukimwi na maambukizi mapya.

Othman aliyasema hayo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani visiwani humo iliyofanyika eneo la Kidimni Wilaya ya Kati, mkoa wa Kusini Unguja chini ya kauli mbiu ya 'Tuweke usawa kumaliza Ukimwi na majanga mengine".

Alisema ni lazima serikali na jamii zikafanya jitihada za pamoja kuhakikisha watu wanapata huduma sawa kwa kuwa bila kufanya hivyo lengo la dunia kutokomeza Ukimwi ifikapo 2030 halitafikiwa.

Aidha, alisema dunia imeweka msisitizo kuhakikisha mataifa yanakuwa kitu kimoja katika kuimarisha upatikanaji wa rasilimali za afya zinazotosheleza wote.

Kwa mujibu wa Makamu huyo, Zanzibar imefanikiwa kupunguza maambukizi mapya kutoka 366 mwaka 2010 hadi 177 mwaka 2021, na kwamba ni hatua nzuri ya kupongezwa na kuongeza jitihada za kujikinga.

Pia , alisema licha ya mafanikio hayo bado hali ya maambukizi kwa makundi maalum siyo ya kuridhisha na kwamba wanahitaji kupewa kipaumbele kwenye elimu na afua mbalimbali.

Kwa upande wa matumizi ya dawa alisema takwimu zinaonyesha wanaojitambua kuwa wanaishi na VVU kwa makundi yao na asilimia kwenye mabano ni wanaotumia dawa za kulevya (48), wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja (60), huku wanawake wanaojiuza (73).

Naye, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid, alisema licha ya takwimu za kitaifa kuonyesha kupungua lakini mkoani humo maambukizi mapya yameongezeka.

Alisema vinavyochochea maambukizi mapya ni upigaji wa ngoma holela za muda mrefu, mikusanyiko ya usiku, baa nyingi za kuuzia pombe na kuwepo vitendo vya kujamiiana kiholela na kwamba zinahitajika jitihada za dhati kuounguza vitendo hivyo.

Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema kwamba serikali inafanya mapitio sera na mikatati ya kupambana na maradhi hayo, ikiwa ni jitihada za kuongeza kasi ya mapambano ya Ukimwi Zanzibar.

Naye, Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Umoja wa Matifa la Kupambana na Ukimwi Duniani (UNAIDS) Zanzibar Dk. Gorge Loy, aliipongeza serikali kwa jitihada za kukabili ugonjwa huo na kuomba kuongeza bidii ili kupunguza maambukizi mapya.

"Katika kupambana na tatizo hilo, hivi sasa duniani kunahitajika juhudi zaidi za pamoja za kuleta mageuzi na mabadiliko ya mifumo ya kisera na kuweka misingi ya usawa katika kulinda haki ya kila mtu, ili kupambana na changamoto zinazojiri katika mapambano dhidi ya Ukimwi,"alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LUIZA A KAKOKELE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato ch a nne chenye **index namba S2214-0048** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary RUNGWA mwaka 2019,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/STA/RB/541055/2021**

116597102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH YESAYA MWAKIBUTI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA VITZ** yenye namba za usajili **T 644 BDW,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/RB/570633/2021**

116597202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MANYONI. Kituo cha KINTINKU Mkoa SINGIDA.**

**Usimamizi wa mirathi Na 04/2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HARBART JOSEPHAT LUNDULLAH WA MAKORONGO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MERIANA NKOMO BATINDA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 mwezi 12 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 29 mwezi 11 mwaka 2021.**

MAHAKAMA YA MWANZO KINTINKU
HAKIMU
RESIDENT MAGISTRATE KINTINKU

116597402

## KUPOETELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ATHUMANI HAMZA SHOMARI** Anatangaza kupotelewa na Kadi yake ya pikipiki aina ya sanlg yenye no za usajili **MC 466AYF,** kwa yeyote akaeiona au kuokota atoe taarifa Kituo chochote Cha polisi au apige Simu namba **0687779727.**
**RB Namba. MOR/MOR/RB/527051/2021**

116597502

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA ARUSHA**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI SHAURI LA MIRATHI NO.31 OF 2021.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA CHANA UKA MODHWADIA......MAREHEMU**

**NA**

**NATHA CHANA MODHWADIA....MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua za usimamizi wa mirathi kwa Mwombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 22 Mwezi wa 2 Mwaka wa 2022.

Imewasilishwa Arusha leo tarehe 26 Mwezi wa 11 mwaka wa 2021.

Imewasilishwa
R. B. Massam
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
ARUSHA

116597602

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANGEL JAMES JOHN** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye **index namba S0239/003** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya skondary ya **ST.FRANCIS GIRLS** mwaka 2015, na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S2325/0506** kilichotolewa na baraza kupitia shule ya secondary ya CANOSSA GIRLS mwaka 2018, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, **DAR/KIJ/RB/570202/2021**

116597302

## KUPOTEA KWA VYETI



**HONEST D MASSAWE** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0629/0133** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **EDMUND RICE** mwaka 2008 na cheti cha kidato cha sita kilichotolewa na baraza kupitia shule ya MAIRIVA HIGH mwaka 2011,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MBU/RB/571995/2021**

116598202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU**
**DAR ES SALAAM**

**SHAURI LA MAOMBI NO 173 YA MWAKA 2021**

**HASSAN MCHANJAMA...........MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MAULID MASALU NA WENZAKE......11 WENZAKE**

KWA,
1.MAULID MASALU, 2.FROLENCE MSILOTWA, 3.DICKSON BWABO, 4.OPTATUS LAURIAN, 5.ANGELA MAZULA, 6.SIMBA ABDUL SIMBA, 7.LAWRENCE SIMO, 8.OBEID LUHWAGO, 9.MODEST NKURLU, 10.MARCEL CYABUKOMBE RUGAMBWA, 11.FREDRICK SIWALE, 12.LEONARD MAPUNDA

**KUITWA SHAURINI**

Kwakuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo ya mwombaji yameelezwa katika nakala ya maombi ambazo zinaweza kupatikana katika mahakama hi,mnahitajika kuhudhuria katika mahakama hii binafsi au wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa kisheria,siku ya tarehe 14/12/2021 saa 07:00 mchana mbele ya Mh.E.M.KASSIAN-PRM
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama itathibitisha kama umepokea kuitwa shaurini,itaweza kutoa hukumu kamka umeshindwa
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama leo hii 17/11/2021

HAKIMU MKAZI MKUU
KISUTU -DAR ES SALAAM

116597902

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**

**Kituo Cha Mjini Mkoa wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na 331/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MOHAMED NASORO WA SABASABA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA PILI ALFANI KUMWEMBE**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 08 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .
Zingatia
Endapo Kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

**Imetolewa Leo 02 Mwezi 12 Mwaka 2021**

116597802

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## UN yaafiki harakati dhidi ya waasi wa ADF

**Kinshasa,** DRC

UJUMBE wa Umoja wa Mataifa (UN), katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), umesema kuwa unaafiki ushiriki wa kikanda wa kukabiliana na tishio linalovuka mipaka la waasi hao.

Kauli hii inakuja baada ya majeshi ya DRC na Uganda, kuanzisha operesheni ya pamoja ya kuwawinda wapiganaji kutoka kikundi cha Allied Democratic Forces (ADF), baada ya kushutumiwa kufanya mashambulio ya kujitoa muhanga katika mji mkuu wa Uganda Kampala, mwezi uliopita.

Majeshi hayo mawili yanafanya operesheni za anga na ardhini, dhidi ya waasi wa ADF.

Msemaji wa UN DRC, Mathias Gillman, aliuambia mkutano wa waandishi wa habari mjini Kinshasa Jumatano kuwa hatua hiyo ni chaguo halali kisheria na uamuzi wa mamlaka za Wacongo.

"Tunazishauri nchi za kanda kushirikiana kutatua tishio linalovuka mpaka. Congo ilichukua uamuzi huo kupambana na ADF, na tunauheshimu," Gillman aliongeza.

Umoja wa Mataifa umekuwa na kikosi cha wanajeshi wake Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), kwa miongo miwili iliyopita.

Mapema mwaka huu, maandamano yalitikisa miji ya Goma na Beni ambapo watu walitoa wito wa kumalizika kwa operesheni za UN, wakisema kuwa umoja huo umedhihirisha kukosa ufanisi, ikatika juhudi za kupata utulivu nchini humo.

Desemba 6, mwaka jana, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limepanga kuamua iwapo kikosi chake kitaendelea kuwapo DRC au la. **BBC**

**Kauli hii inakuja baada ya majeshi ya DRC na Uganda, kuanzisha operesheni ya pamoja ya kuwawinda wapiganaji kutoka kikundi cha Allied Democratic Forces (ADF), baada ya kushutumiwa kufanya mashambulio ya kujitoa muhanga katika mji mkuu wa Uganda Kampala, mwezi uliopita.**

# UN, AU walaani ubaguzi unaoathiri Afrika

**New York,** MAREKANI

UMOJA wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) kwa pamoja wamelaani ubaguzi ambao baadhi ya nchi za Kusini mwa Afrika zimekuwa zikifanyiwa, kwa kuwa zinakabiliwa na kirusi kipya cha Omicron.

Mwenyekiti wa Tume ya AU alikuwa UN na kukutana na katibu mkuu kwa mkutano wao wa kila mwaka.

Ni habari iliyochukua nafasi ya kwanza kuliko tafakari zao za kawaida za kidiplomasia.

Antonio Guterres na Moussa Faki Mahamat, wamejitokeza pamoja kwa kuelezea hisia zao, kutokana na hatua ya kufungwa kwa mipaka iliyotangazwa na nchi mbalimbali duniani.

Katibu Mkuu wa UN alisisitiza kuwa Afrika imehukumiwa mara mbili katika janga hili, kwa kukosa kupata chanjo za kutosha kwanza, na kwa sasa kukwama katika kufufua uchumi wake.

"Tuna vifaa vya kusafiri kwa usalama. Basi tuvitumie vyombo hivi ili kuepukana na hali hii...kama mtaniruhusu niseme hivyo...ubaguzi wa kusafiri! "

Mwenyekiti wa AU, Moussa Faki Mahamat, pia amezishambulia nchi hizo kwa maeneo makali. Hasa wakati hatua hizi zinachukuliwa wakati huu wa sherehe za majira ya joto na mwisho wa mwaka.

"Ilibainika kuwa virusi hivi vilikuwapo katika nchi moja au mbili za Ulaya muda mrefu kabla ya ugunduzi uliofanywa na Afrika Kusini," Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika alisema.

Moussa Faki Mahamat, alieleza kuwa shirika lake, WHO na Mamlaka ya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa barani Afrika (CDC), wanafanya kinachowezekana kuyafanya mataifa haya kuelewa kwamba, kisayansi vikwazo hivyo havina uhalali, wakitumaini kwamba vitaondolewa hivi karibuni.


Wakati huo huo, Mamlaka ya Usimamizi wa Dawa Uingereza, imeidhinisha dawa zinazozalishwa na kampuni ya GlaxoSmithKline, GSK kutibu kundi lililo hatarini kupata dalili mbaya za maambukizi ya COVID-19.

Kampuni hiyo ya GlaxoSmithKline ilisema dawa yake imeonekana kuwa na ufanisi wa kukabiliana na kirusi kipya aina ya Omicron.

Kampuni hiyo ya GSK ilisema takwimu ya kitiba za wali zimeonyesha kwamba tiba ya sotrovimab hudhoofisha nguvu ya kirusi hicho kujibadilisha na kuongeza kuwa majaribio bado yanaendelea, ikitaraji kutoa matokeo kamili ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Dozi moja ya dawa hiyo ilionekana kupunguza hatari ya wagonjwa kulazwa hospitalini na vifo kwa asilimia 79 kwa watu wazima walio katika hatari kubwa ya kupata kuambukizwa Covid-19.

**UN/DW**



Mwanaume akipiga picha moja ya meli ambazo zimekwama kwenye ufu wa bahari ya Marmara baada ya upepo mkali kuziondoa kwenye ukingo katika Wilaya ya Maltepe mjini Istanbul, nchini Uturuki. **PICHA: REUTERS**

# Wananchi Gambia wajivunia kupiga kura kwa kutumia gololi

**Banjul,** GAMBIA

WAGAMBIA watakapopiga kura kesho, kumchagua rais, karatasi za kupigia kura hazitatumika badala yake zitatumika gololi.

Badala yake, mpigakura akifika katika kituo cha kupigia kura, na baada ya kitambulisho chake kuthibitishwa, ataelekezwa kwenye safu ya ngoma zilizopakwa rangi za vyama vya wagombea tofauti.

Gololi ikitumbukizwa itatoa mlio wa kengele ili viongozi waweze kusikia kama kuna mtu yeyote atajaribu kupiga kura zaidi ya mara moja.

Wakati shughuli ya kupiga kura inapokamilishwa, gololi kutoka kwa kila pipa zinahesabiwa na kujumuishwa, inavyofanywa karatasi za kupiga kura.

Njia hii ya upigaji kura ilianzishwa baada ya uhuru mwaka 1965 kwa sababu ya kiwango cha juu cha watu wasiojua kusoma na kuandika nchini Gambia.

Marekebisho kadhaa yamefanywa tangu Yayha Jammeh kuondoka madarakani baada ya kushindwa katika uchaguzi wa rais mwaka 2016.

Baadhi ya maofisa wa uchaguzi kisiri kuwa na matumaini kwamba mfumo wa upigaji kura kupitia gololi ungelikuwa moja ya mabadiliko hayo.

Walikuwa wanahoji kwa misingi ya kupanuka kwa nafasi ya kidemokrasia na uwezekano wa wagombea wengi kushiriki katika chaguzi zijazo, hivyo basi mfumo wa kupiga kura kwa kutumia gololi na ngoma unaweza kuwa mgumu sana na wa kuchosha.

Zamani ni ngoma tatu tu zilihitajika katika kila kituo cha kupigia kura.

Wakati wa miaka 22 ya Jammeh mamlakani ilionekana kuwa na umuhimu mdogo katika kugombea.

Gambia imekuwa na marais watatu tu katika historia yake.

**BBC**

# YANGA YAANZA HESABU LEO KUMKABILI MNYAMA

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji wa Yanga kinatarajiwa kuingia kambini leo jioni kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya watani zao, Simba itakayochezwa Desemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema baada ya mapumziko ya siku mbili, tangu kumalizika mechi dhidi ya Mbeya Kwanza kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, kikosi hicho kitaanza mazoezi mengine maalumu kuelekea mchezo huo utakaowakutanisha wakongwe wawili.

Bumbuli alisema programu rasmi kuelekea 'dabi' hiyo ya kwanza msimu huu yataanza kufanyika jioni na benchi la ufundi liko tayari kwa kazi hiyo.

"Ijumaa jioni ndio tutaanza kujiandaa kwa ajili ya mchezo wetu unaofuata wa ligi, huku madaktari wetu wakiendelea kuwafuatilia wachezaji ambao ni majeruhi, lakini tunashukuru sana wanachama na mashabiki kwa ushirikiano na umoja wao kwani umetufanya tukusanye pointi saba za ugenini, licha ya kwamba lengo letu lilikuwa ni pointi tisa," alisema Bumbuli.

Kiongozi huyo alisema mechi iliyowaharibia ilikuwa ni dhidi ya Namungo ambayo walilazimishwa sare ya bao 1-1, akiahidi kubeba pointi zote tisa katika michezo yao mitatu watakayocheza mwezi huu.

Aliongeza mbali na kujiandaa na michezo ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, pia wanajiweka tayari kufanya vizuri katika mechi yao ya mashindano ya Kombe la FA ili wasonge mbele kwenye michuano hiyo inayochezwa kwa njia ya mtoano.

"Ratiba inaonyesha Desemba tuna mechi tatu za ligi na moja ya FA, tumejiandaa kupata pointi tisa na kufuzu hatua inayofuata katika Kombe la FA," Bumbuli alisema.

Wakati huo huo, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imesema hatua ya Yanga kukaa muda mrefu bila kucheza mechi yoyote kunatokana na ratiba ilivyotengenezwa awali wakati timu hiyo ilipokuwa inashiriki michuano ya kimataifa.

Ofisa Habari wa TPLB, Karim Boimanda, alisema awali ratiba ilipangwa kwa kuweka nafasi ili timu zishiriki michuano ya kimataifa hadi kufikia fainali.

"Simba na Yanga kwenye Ligi ya Mabingwa na Azam na Biashara United kwenye Kombe la Shirikisho, hizi siku ambazo unaona ziko wazi ni zile ambazo zilipaswa kucheza mechi za kimataifa kama wangekuwa hawajatolewa," alisema Boimanda.

Hata hivyo, Yanga itakuwa na faida ya kuwa na muda mrefu wa kufanya maandalizi ya kuikabili Simba ambayo keshokutwa itakuwa ugenini Lusaka, Zambia kurudiana na Red Arrows kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.




Kamishna Somoe Ng'itu (katikati), akiwa na waamuzi na manahodha kabla ya mechi ya kirafiki ya kimataifa kati ya mabingwa wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, Simba Queens dhidi ya wenzao kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), FCF Amani. Simba Queens ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Ushindi wa Biko watua Lugoba

**Mwandishi Wetu, CHALINZE**

MKAZI wa Lugoba, wilayani Chalinze mkoani Pwani, Hashimu Shabani, amekabidhiwa Sh. milioni 10 alizoshinda kutoka kwenye droo kubwa ya bahati nasibu ya Biko, ambayo inayoongoza kutoa washindi wengi kutoka sehemu mbalimbali.

Makabidhiano hayo yamefanyika Pwani na kuongozwa na balozi wa Biko, Kajala Masanja ambaye alisema mchezo huo unaosambaza mamilioni ya fedha kwa Watanzania wanaocheza 'live' kwa njia ya mtandao www.biko.co.tz pamoja na wanaotumia namba ya Kampuni 505050 na kumbukumbu 2456 au neno biko.

Akizungumza baada ya makabidhiano, Shabani alisema fedha alizopata ataziingiza kwenye mradi wake wa kumiliki bodaboda ili zimsaidie katika maisha yake huku akiamini bahati kama hiyo inaweza isijirudie tena.

"Namshukuru Mungu kwa kunipatia fursa hii ya kushinda zawadi nono ya Sh. milioni 10 kutoka kwenye bahati nasibu ya Biko, hivyo wakati huu ambao maisha ni magumu mtaani, nimeamua kununua bodaboda nikiamini zinaweza kuniokoa.

"Siwezi kufanya makosa, maana Mungu mwenyewe ndiye anayejua kwanini ameamua kunipa ushindi wa Biko, ingawa nilicheza nikiwa na imani kubwa kama kuna siku ningeweza kuibuka mshindi kama wanavyoshinda wengine," alisema Shabani.

Naye Masanja alisema wakati huu wa kuelekea kufunga mwaka, Watanzania wote wanaocheza Biko wana nafasi kubwa ya kushinda zawadi za papo kwa hapo pamoja na ofa kibao zikiwamo za mamilioni kila Jumapili.

## Simba, Yanga, Mbeya City safi

**Na Adam Fungamwango**

MPAKA raundi ya saba inamalizika, Simba, Yanga na Mbeya City, ndio timu pekee ambazo hazijapoteza mechi yoyote katika Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, huku Ruvu Shooting ambayo leo itacheza dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Mabatini Mlandizi mkoani Pwani ikiwa ndiyo timu pekee ambayo haijatoa sare yoyote.

Yanga ambayo inaongoza ligi ikiwa na pointi 19, imecheza mechi saba, ikishinda michezo sita na kutoka sare moja tu, huku watani wao wa jadi, Simba wakicheza mechi kama hizo, wakishinda tano na kutoa sare mechi mbili.

Mbeya City ambayo haitazamwi na wengi, lakini takwimu zinaonyesha imecheza mechi saba, imeshinda mechi mbili na kutoka sare mara tano, pia ikishika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi kwa pointi 11.

Ruvu Shooting yenyewe ndiyo timu pekee ambayo haijatoka sare hata mara moja, ikiwa tayari imecheza mechi saba, imeshinda mechi tatu na kupoteza nne, ikikamata nafasi ya saba baada ya kujikusanyia pointi tisa. Mtibwa Sugar yenye pointi mbili, yenyewe imeweka rekodi ya kuwa timu pekee kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara mpaka sasa haijashinda mchezo hata mmoja na inaburuza mkia katika msimamo.

## KMKM yatamba kuendeleza ubabe

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA watetezi, KMKM imesema imejipanga kuhakikisha inaendelea kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu ya PBZ Zanzibar kwa sababu inahitaji kuona inanyakua tena ubingwa wa ligi hiyo msimu huu, imefahamika.

KMKM ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 21, baada ya kushinda michezo sita na kutoka sare tatu.

Hata hivyo, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, amesema ligi hiyo msimu huu ni ngumu lakini wataendelea kupambana katika kila mzunguko watakaocheza.

Msimu alisema licha ya kufanya vizuri katika michezo iliyopita, bado anakiri ligi ni ngumu na ni mapema kutabiri bingwa kwa sababu hawana uhakika wa ushindi wa michezo iliyoko mbele yao.

"Tunapambana ili kufikia malengo ya kutetea ubingwa yatimie, lakini ligi bado ni ngumu sana, michezo tisa tuliocheza ni mingi kwa hesabu lakini utaona ni midogo kwa matokeo ya uwanjani, udhamini uliopo umeongeza changamoto," alisema Msimu.

Aliongeza amejiandaa kukutana na ushindani kwenye mchezo wao unaofuata dhidi ya Malindi utakaochezwa Desemba 5, mwaka huu kutokana na wapinzani wao hao kupoteza mechi mbili za nyuma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEWANDOWSKI AITAKA MADRID
REAL Madrid ndio mahali anapopendelea zaidi, Robert Lewandowski iwapo mshambuliaji huyo wa Poland mwenye umri wa miaka 33, ataondoka Bayern Munich msimu ujao wa joto. **(AS)**

### AZPILICUETA ANUKIA BARCA
BARCELONA wanataka kumsajili mlinzi wa Hispania, Cesar Azpilicueta kwa uhamisho huru. Nahodha huyo wa Chelsea mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto unaokuja .**(Marca)**

### BENITEZ MAMBO MAGUMU
EVERTON wanaweza kumfuta kazi kocha, Rafael Benitez au Mkurugenzi wa Soka, Marcel Brands wakati wowote kuanzia sasa. **(Football Insider)**

### RANGNICK AMTAKA WERNER
KOCHA mpya wa muda, Ralf Rangnick anatamani Manchester United kufanya usajili wa mshambuliaji wa Chelsea na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, majira ya joto. **(Bild, via 90min)**

### HAALAND KUMBEBA RANGNICK
RALF Rangnick atapokea bonasi ya euro milioni 10 ikiwa atamshawishi mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, kujiunga na Manchester United. **(Bild)**

### UNITED YATENGA FUNGU
KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick atapewa bajeti ya uhamisho ya hadi pauni milioni 100 ili kuimarisha kikosi cha Mashetani Wekundu hao Januari. **(Mirror)**

### MUKIELE ANUKIA EPL
MLINZI wa kulia wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Nordi Mukiele mwenye umri wa miaka 24, anafuatiliwa na Manchester United. **(90min)**

### ZIYECH AWEKWA SOKONI
CHELSEA wako tayari kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Morocco, Hakim Ziyech mwenye umri wa miaka 28 na mshambuliaji wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, kwenda Barcelona. **(Sport)**

### JORGINHO MAMBO BADO
WAKALA wa Jorginho amesema kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Italia mwenye umri wa miaka 29 hajafanya mazungumzo na Chelsea kuhusu kuongeza mkataba mpya.**(Tuttomercatoweb)**

### HEE-CHAN KUTUA LEICESTER
KLABU ya Leicester City wanapanga kumnunua mshambuliaji wa Wolves, Hwang Hee-chan mwenye umri wa miaka 25 ifikapo Januari. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini yuko kwa mkopo hapo Molineux kutoka RB Leipzig.**(Football insider)**

### NUNEZ KUTUA DORTMUND
BORUSSIA Dortmund imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, kutoka Benfica. **(Record)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: CHELSEA FC HATUKUSTAHILI USHINDI

●●●Kocha huyo afunguka kikosi chake kilicheza chini ya kiwango na...

**LONDON, England**

THOMAS Tuchel anahisi Chelsea "waliiba pointi tatu" kwa ushindi wao wa mabao 2-1 dhidi ya Watford, hapo juzi Jumatano.

The Blues hao hawakuwa katika kiwango chao cha kuvutia pale kwenye dimba la Vicarage Road.

Walikamilisha asilimia 71 ya uhakika wa pasi zao na ilikuwa ni ya chini zaidi ya Tuchel kwenye mashindano yote na mbaya zaidi tangu walipocheza na Liverpool kwenye Ligi Kuu England, Mei mwaka, 2018.

Mason Mount aliwaweka mbele baada ya bao la dakika ya 30 wakati shabiki mmoja aliripotiwa kupatwa na shambulio la moyo - na baadaye Watford walithibitisha wameimarika.

Hata hivyo, Emmanuel Dennis alikuwa mchezaji wa kwanza wa Watford kufunga katika mechi tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu England tangu Troy Deeney alipofanya hivyo mwaka 2017 wakati aliposawazisha kabla ya kipindi cha pili.

Vijana wa Tuchel walionekana kama wameacha pointi moja kwa mara ya tatu kwenye Ligi Kuu England, lakini Hakim Ziyech aliyetokea benchi aliwezesha ushindi wa tatu mfululizo hapo kwenye dimba la Vicarage Road kwa mara ya kwanza kwenye historia ya Chelsea.

"Tuliiba pointi tatu. Hatutakiwi kuzungumza kuhusu hilo. Kwa mara ya kwanza nahisi tulikuwa na bahati kupata ushindi," alisema Tuchel, ambaye alifanya mabadiliko sita, akiambia Amazon Prime.

"Wale sio sisi. Kwa uhakika kabisa hatukuwa tayari kwa mchezo wa leo (juzi). Pengine nilishindwa kupata namna nzuri ya mbinu kwa mchezo huu. "Naamini kabisa hatukuwa kwenye ubora tuliotakiwa kuwa nao, naamini tulikuwa mbali kabisa na kiwango chetu.

"Lakini jambo la msingi ni kwamba, tulikuwa na bahati kupata pointi tatu na hilo ndilo lilikuwa jambo la muhimu zaidi kwetu."

MECHI KALI
HOME
AWAY
FULHAM
1.88 | 3.53 | 3.77
BOURNEMOUTH
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 735
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KLOPP AWAVULIA KOFIA SALAH, MANE

**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp alimsifia shujaa wake wa mabao wawili, Mohamed Salah na Sadio Mane baada ya wekundu hao kuifumua Everton mabao 4-1 katika mchezo wa dabi ya jiji moja hapo juzi usiku.

Salah alifunga mara mbili wakati Liverpool ikiifunga Everton kwenye Ligi Kuu England pale katika dimba la Goodison Park, Jumatano.

Jordan Henderson na Salah walianza kufunga mabao ya ufunguzi ndani ya dakika 20 za mwanzo na huku Demarai Gray akiifungia bao Everton kuelekea kipindi cha pili.

Liverpool walijihakikishia ushindi baada ya Salah kufunga bao lake la pili na la tatu kwa timu kabla ya Diogo Jota kufunga la nne.

Salah amefunga mabao 13 kwenye Ligi Kuu England msimu huu, tisa kati yake akiyafunga ugenini.

Pia Salah alikuwa mchezaji wa kwanza wa Liverpool kufunga mara mbili ugenini dhidi ya Everton tangu Fernando Torres alipofanya hivyo, Septemba, mwaka 2008.

Klopp alimsifia Salah, Mane na Jota baada ya mchezo huo ambao sasa umewafanya Liverpool kuwa katika nafasi tatu wakipitwa pointi mbili na vinara Chelsea.

"Sio yeye tu, lakini yeye alifanya kazi nzuri zaidi," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari wakati alipoulizwa kuhusu Salah.

"Kufunga mabao mawili kama haya, la kwanza ilikuwa pasi kutoka kwa Hendo (Jordan Henderson) na lile jingine...alifanya (Seamus) Coleman kuwa chini ya presha."



# Lewandowski afikiriwa kupewa Ballon d'Or 2020

**PARIS, Ufaransa**

WAANDAAJI wa tuzo za Ballon d'Or wameeleza wanafikiria kuhusu kumzawadia, Robert Lewandowski tuzo ya mwaka 2020 baada ya kauli ya Lionel Messi aliyotoa kwenye sherehe hizo alipopokea tuzo yake ya saba.

Kutokana na mlipuko wa virusi vya corona mwaka 2020, tuzo za Ballon d'Or hazikutolewa kwa mchezaji yeyote baada ya waandaji kuzifuta kwa mwaka huo.

Lewandowski alikuwa kwenye kiwango kizuri akiwa na timu yake ya Bayern Munich aliyoisaidia kuchukua mataji matatu likiwamo Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Lewandowski Robert, ulistahili tuzo yako ya Ballon d'Or mwaka uliopita, kila mmoja alikubali kuwa wewe ndiye ulikuwa mshindi wa hii tuzo. Natumaini waandaji watakupa Ballon d'Or ya 2020. Wote tunaamini unastahili hiyo na natumai utakuwa nayo nyumbani," alisema Messi wakati akitoa neno la shukrani.

Lewandowski alikuwa na msimu mzuri pia aliweza kuchukua tuzo ya mchezaji bora wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na kufanikiwa kufunga mabao 55.

Pia Lewandowski hadi sasa amefunga mabao 25 katika michezo 20, alikubali kuwa kipindi tuzo zinaahirishwa mwaka uliopita alikuwa kwenye kiwango bora kabisa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mwandaaji wa tuzo hiyo, Pascal Ferre ilisema: "Hatuna haraka ya kufanya uamuzi, tunaweza kufikiria hili kwa kina. Hatuwezi kuwa na uhakika kama Lewandowski angeshinda Ballon d'or mwaka uliopita, sababu kulikuwa hakuna kura iliyopigwa."

5,865,580

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 04/12/21 | 18:00 | Blackpool vs Luton Town | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 02. 04/12/21 | 18:00 | Reading vs Hull City | 2.35 | 3.23 | 2.89 |
| 03. 04/12/21 | 18:00 | Bristol City vs Derby | 2.40 | 3.14 | 2.89 |
| 04. 04/12/21 | 18:00 | Barnsley vs Huddersfield | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 05. 04/12/21 | 18:00 | Newcastle vs Burnley | 2.24 | 3.31 | 3.21 |
| 06. 04/12/21 | 18:00 | Southampton vs Brighton | 2.42 | 3.30 | 2.90 |
| 07. 04/12/21 | 23:00 | Real Sociedad vs Real Madrid | 3.01 | 3.26 | 2.37 |
| 08. 05/12/21 | 14:30 | Bologna vs Fiorentina | 2.56 | 3.51 | 2.61 |
| 09. 05/12/21 | 16:00 | Rayo Vallecano vs Espanyol | 2.30 | 3.15 | 3.25 |
| 10. 05/12/21 | 17:00 | Lorient vs Nantes | 2.84 | 3.24 | 2.48 |
| 11. 05/12/21 | 17:30 | QPR vs Stoke City | 2.36 | 3.23 | 2.89 |
| 12. 05/12/21 | 19:30 | Aston Villa vs Leicester | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 13. 05/12/21 | 20:30 | Levante vs Osasuna | 2.45 | 3.20 | 2.95 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 03 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2140 | Bahrain vs Iraq | 2.99 | 2.79 | 2.46 |
| 13:00 | 3682 | Junior Sevan vs Pyunik Yerevan | 3.08 | 3.18 | 2.17 |
| 16:00 | 1737 | Brighton U23 vs Liverpool U23 | 1.82 | 3.81 | 3.47 |
| 16:00 | 3815 | Oman vs Qatar | 6.35 | 3.51 | 1.52 |
| 16:00 | 5878 | Wigan U23 vs Barnsley U23 | 1.89 | 3.95 | 3.55 |
| 17:20 | 2572 | AL Tadamon vs Yarmouk | 2.23 | 3.47 | 2.75 |
| 17:30 | 1101 | Urartu vs Ararat Armenia | 5.02 | 3.57 | 1.61 |
| 18:00 | 2592 | Shakhtar Donetsk vs FK Lviv | 1.11 | 6.92 | 17.29 |
| 19:00 | 2406 | Zenit St Petersburg vs Rostov | 1.20 | 6.28 | 11.77 |
| 19:00 | 3754 | Mauritania vs United Arab Emirates | 8.80 | 4.40 | 1.39 |
| 20:00 | 4366 | Stal Mielec vs Wisla Plock | 2.51 | 3.14 | 2.61 |
| 20:00 | 4629 | Kasimpasa vs Besiktas | 3.55 | 3.74 | 1.90 |
| 20:00 | 5388 | Aris Limassol vs Olympiakos Nicosia | 2.08 | 3.37 | 3.42 |
| 20:30 | 1392 | Hobro vs FC Helsingor | 5.60 | 4.34 | 1.45 |
| 20:30 | 1713 | Werder Bremen vs Erzgebirge Aue | 1.49 | 4.31 | 5.68 |
| 20:30 | 2204 | SV Darmstadt vs Fortuna Dusseldorf | 1.93 | 3.63 | 3.48 |
| 20:30 | 3906 | FC Fredericia vs Horsens | 3.03 | 3.61 | 2.03 |
| 21:00 | 1015 | Boulogne vs Laval | 2.70 | 3.04 | 2.60 |
| 21:00 | 4267 | Chambly vs Sedan | 2.16 | 2.93 | 3.57 |
| 22:00 | 1240 | MSK Deinze vs Excelsior Virton | 1.36 | 4.90 | 6.85 |
| 22:00 | 2078 | Maastricht vs FC Oss | 2.73 | 3.55 | 2.29 |
| 22:00 | 2096 | Dordrecht vs Roda Kerkrade | 5.25 | 4.67 | 1.47 |
| 22:00 | 2850 | Groningen vs PEC Zwolle | 1.80 | 3.53 | 4.12 |
| 22:00 | 3671 | Den Bosch vs NAC Breda | 3.46 | 3.85 | 1.86 |
| 22:00 | 4696 | Almere City vs FC Eindhoven | 2.10 | 3.61 | 3.02 |
| 22:00 | 4985 | Telstar vs VVV Venlo | 2.13 | 3.57 | 2.99 |
| 22:00 | 5729 | Helmond Sport vs FC Volendam | 5.25 | 4.67 | 1.47 |
| 22:00 | 5887 | Syrian Arab Republic vs Tunisia | 5.18 | 3.41 | 1.63 |
| 22:00 | 5934 | Portimonense vs Porto | 7.69 | 4.64 | 1.37 |
| 22:30 | 1717 | Union Berlin vs RB Leipzig | 3.84 | 3.64 | 1.89 |
| 22:30 | 1973 | FC Aarau vs FC Winterthur | 2.03 | 3.42 | 3.18 |
| 22:30 | 2584 | Yverdon-Sport FC vs FC Schaffhausen | 2.45 | 3.42 | 2.50 |
| 22:30 | 4479 | Perugia vs Vicenza | 1.82 | 3.34 | 4.33 |
| 22:45 | 1682 | St Truiden vs Union Saint Gilloise | 3.95 | 3.85 | 1.78 |
| 22:45 | 3303 | Rotherham vs Stockport | 1.48 | 4.24 | 6.12 |
| 22:45 | 3481 | Lynx FC vs Europa Point FC | 1.02 | 13.52 | 20.28 |
| 22:45 | 3751 | Inverness vs Kilmarnock | 2.40 | 3.18 | 2.84 |
| 22:45 | 4974 | Bala Town vs The New Saints | 5.60 | 4.40 | 1.54 |
| 22:45 | 5533 | Fulham vs Bournemouth | 1.88 | 3.53 | 3.77 |
| 22:45 | 5876 | Gateshead vs Charlton | 5.35 | 4.46 | 1.51 |
| 23:00 | 2122 | Huesca vs Valladolid | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 23:00 | 2216 | AC Ajaccio vs Valenciennes | 1.81 | 3.34 | 4.42 |
| 23:00 | 3860 | Paris FC vs Bastia | 2.02 | 3.19 | 3.68 |
| 23:00 | 3881 | Sochaux vs PAU FC | 1.97 | 3.14 | 3.93 |
| 23:00 | 3883 | Guingamp vs Dijon | 2.46 | 3.05 | 2.90 |
| 23:00 | 3898 | US Quevilly Rouen vs Nancy | 2.60 | 2.95 | 2.80 |
| 23:00 | 4231 | Granada vs Alaves | 2.53 | 3.08 | 2.93 |
| 23:00 | 4731 | Rodez Aveyron vs Nimes | 2.51 | 2.96 | 2.91 |
| 23:00 | 4748 | Amiens vs Dunkerque | 2.19 | 2.94 | 3.53 |
| 23:00 | 5916 | Grenoble Foot vs Le Havre | 2.46 | 2.95 | 3.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MINZIRO ALILIA BAO LILILOKATALIWA

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Geita Gold FC, Fred Minziro amelalamika kunyimwa bao walilolipata dhidi ya Simba katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, iliyochezwa kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam, juzi.

Mabingwa watetezi, Simba waliendeleza furaha kwa mashabiki wao baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Geita Gold, lakini Minziro anaamini walionewa.

Mabao ya Simba yalifungwa na viungo, Mmalawi Peter Banda dakika ya tisa na mzawa, Muzamiru Yassin dakika ya 57, wakati la Geita Gold lilifungwa na Juma Mahadhi dakika ya 66 wakati lile la George Mpole likikataliwa kwa sababu mfungaji alifanya madhambi kabla ya kufunga.

Na sasa Minziro ameonekana kumtupia lawama mwamuzi wa mchezo huo, Martin Saanya, akidai aliwapendelea Simba kwa kukataa bao lao la wazi.

Alisema Geita Gold walipaswa kupata angalau pointi moja kwenye mchezo huo, na kukataliwa kwa bao hilo kumewafanya wapoteze pointi zote tatu.

"Nyinyi wenyewe waandishi mnaweza kuangalia vizuri tu marudio kwenye televisheni, tulinyimwa bao letu la wazi kabisa," alisema Minziro.

Kwa ushindi huo, Simba imefikisha pointi 17, ingawa inabaki katika nafasi ya pili ikizidiwa pointi mbili na vinara Yanga baada ya timu zote kucheza mechi saba.




Kipa wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite), Husna Mtunda akipangua mpira kwenye mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Burundi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# Metacha afunguka Polisi Tz inakamiwa

**Na Dennis Fussi**

GOLIKIPA chaguo la kwanza wa Polisi Tanzania, Metacha Mnata amesema timu yao imekuwa 'ikikamiwa sana' kwa sababu ilianza vizuri kwenye Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara msimu huu.

Metacha amesema tangu washinde mechi tatu mfululizo za kwanza timu nyingi wanazokutana nazo zimekuwa zikiwakamia kiasi cha kushindwa kuonyesha kiwango chao na kujikuta wakipata sare au kupoteza mchezo.

Nyota huyo alisema wamekuwa wakijipanga kuhakikisha wanaendeleza ubora waliokuwa nao kwenye mechi za kwanza za msimu huu, ili kujiweka kwenye nafasi nzuri katika mbio za kuwania ubingwa.

"Ligi Kuu msimu huu ni ngumu sana, lakini pamoja na ugumu huo timu nyingi zinatukamia sana, lakini sisi wachezaji tutaendelea kupambana ili kuipigania timu yetu," amesema Metacha.

Kipa huyo ambaye msimu uliopita aliidakia Yanga, amesema pamoja na changamoto hizo kutoka kwa timu pinzani lakini wamejizatiti kuhakikisha wanafanya vizuri na kushika nafasi za juu kama ilivyo sasa.

Polisi Tanzania inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuwakabili 'Maafande' wenzao wa Prisons.

Michezo
Ijumaa Desemba 3, 2021
Nipashe



## Tuchel: Chelsea FC hatukustahili ushindi




Kiungo wa Simba, Jonas Mkude (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Geita Gold FC, Danny Lyanga katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 2-1. **PICHA: SIMBA SC**

# Nabi kuendelea kuipangua Yanga

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumaliza mapumziko ya siku mbili, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema ameanza 'kukuna kichwa' namna atakavyowakabili watani zao, Simba katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa Desemba 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Nabi aliliambia gazeti hili ameandaa 'mipango' tofauti kwa ajili ya kuhakikisha kikosi chake kinaendelea kupata matokeo mazuri kwenye mechi mbalimbali za ligi hiyo.

Kocha huyo alisema anatambua Simba ina kikosi imara na kwa sababu hiyo wanatakiwa kujiimarisha zaidi kuhakikisha wanakwenda kutimiza malengo yao kwa kuondoka na ushindi.

"Mchezo hautakuwa rahisi, hatutaingia kwa mbinu tulizokuwa nazo katika mchezo wa kwanza ambao tuliwafunga katika Ngao ya Jamii, hata wao watakuja kivingine na hawatakubali kupoteza mara mbili, watataka kulipa kisasi," Nabi alisema.

Naye Kocha wa Viungo wa Yanga, Helmy Gueldish, alisema anaendelea kutekeleza majukumu kwa kuhakikisha kila mchezaji anafuata masharti ili kuendana na kasi wanayoitaka ili kurejesha heshima ya klabu yao katika msimu huu.

"Kila mechi kwetu ni fainali, hakuna mechi rahisi, wachezaji wanatakiwa kujitambua na kuonyesha nidhamu katika kila mchezo ili kufikia malengo tutayoyatarajia, tutafanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa wapinzani wetu ," aliongeza kocha huyo.

Yanga inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 19 baada ya kushinda michezo sita na kutoka sare mechi moja wakati mabingwa watetezi, Simba wako katika nafasi ya pili wakiwa na alama 17.

# KIWANGO SIMBA CHAMKERA PABLO

## ●●● Aahidi mabadiliko wakiifuata Red Arrows, FCC yaishika GSM...

**Saada Akida na Mary Geofrey**

LICHA ya kupata ushindi wa mabao 2-1, dhidi ya Geita Gold FC, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema hajaridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake na wakiendelea hivyo, watapata shida katika mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Red Arrows ya Zambia.

Simba, wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa watashuka ugenini keshokutwa kuwakabili Red Arrows huku wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 3-0, waliopata Jumapili iliyopita hapa nyumbani.

Pablo alisema kitu pekee alichokipenda katika mchezo huo wa juzi ni kitendo cha kuvuna pointi tatu lakini hajaridhishwa na kiwango walichokionyesha wachezaji wake.

"Hatukuwa bora, tumecheza mchezo mbovu licha ya kushinda, tumeshindwa kutawala mpira na kuwafanya wapinzani watawale mpira, tulitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia, tunaenda Zambia, kwa mwendo huu basi tutakuwa na shida sana, suala la mabadiliko ya kikosi sio sababu," alisema Pablo.

Kocha huyo aliongeza atakwenda kufanyia kazi mapungufu hayo ili kuhakikisha kila mchezaji anafanya vyema majukumu yake kwa ajili ya michezo miwili iliyopo mbele yao ikiwamo dhidi ya JKT Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema wamejipanga vizuri kuelekea mchezo huo dhidi ya Red Arrows na kuhusu suala la 'fitna na mchezo mchafu' pia watapambana nalo.

"Mikakati yetu ni siri kubwa, mashabiki watambue timu yetu ni imara na wachezaji wanatakiwa kufanya majukumu yao, suala la nje ya uwanja ikiwamo fitna hatuna mashaka na hilo kwa sababu tuna uzoefu mkubwa katika michuano ya kimataifa," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kikosi cha Wekundu wa Msimbazi kinatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Zambia ambapo mshindi wa jumla wa mechi hiyo atatinga hatua za makundi.

Aliongeza hawezi kuweka wazi mikakati yao, lakini tayari benchi la ufundi na wachezaji wao wameshajipanga kuhakikisha wanapata ushindi ugenini na hatimaye wanasonga mbele katika michuano hiyo.

Wakati huo huo, kiungo mshambuliaji wa Simba, Bernard Morrison ameteuliwa kuwa Mchezaji Bora wa mashabiki wa Novemba akiwashinda Meddie Kagere na Jonas Mkude.

Kutokana na ushindi huo, Morrison ambaye kwa Novemba alicheza dakika 235 na kufunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho mbili, alikabidhiwa kitita cha Sh. milioni mbili na wadhamini wa tuzo hizo, kampuni ya Emirate Aluminum ACP.

Katika hatua nyingine, Tume ya Taifa ya Ushindani (FCC), imepokea malalamiko kuhusu kampuni ya GSM, kudhamini Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Ushindani Duniani, Mkurugenzi Mkuu wa FCC, William Urio, alisema tume hiyo italitolea ufafanuzi suala hilo baada ya kupitia vielelezo muhimu kuhusiana na mkataba huo ambao GSM wameingia na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Urio alisema FCC ilipokea malalamiko hayo Jumatatu na barua ilieleza GSM itadhamini vipi ligi hiyo huku pia ni wadhamini wakuu wa Yanga.

"Jumatatu tulipokea malalamiko ya kujua kama kitendo hicho hakitaathiri ushindani wa Ligi Kuu. Hilo siwezi kulisema kwa sasa kwa sababu tumeanza kulifanyia kazi na baada ya kulipitia kwa kina tutalitolea taarifa rasmi," alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema suala hilo sio la kushtukiza na wao ni kama mahakama, hivyo wanasikiliza malalamiko na kuyafanyia kazi kikamilifu.

"Mimi binafsi sijaona huo mkataba unasemaje zaidi niliona tu picha kwenye mitandao, tutaomba mkataba walioingia tuuone unasemaje," aliongeza Urio.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >